MFUMO TATHMINI WA TAARIFA ZA OGP:

TANZANIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI 2014–2015

Ngunga Greyson Tepani
Mtafiti Anayejitegemea
Taarifa ya Utekelezaji
Second Progress Report

Open Government Partnership
INDEPENDENT REPORTING MECHANISM

This work is licensed under the Creative Commons Attribution 4.0 International License. To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Open Government Partnership

MFUMO TATHMINI WA TAARIFA ZA OGP:

TANZANIA

TAARIFA YA UTEKELEZAJI 2014-2015

EXECUTIVE SUMMARY 3

MUHTASARI: TANZANIA 9

I | USHIRIKI KATIKA OGP KITAIFA 15

II | MCHAKATO: UANDAAJI WA MPANGO KAZI 17

III | UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI 21

IV | UCHAMBUZI WA YALIYOMO KWENYE MPANGO KAZI 23

3.1 | UPATIKANAJI TAARIFA 27

3.2 | TAKWIMU HURIA 30

3.3 | UWAZI KATIKA BAJETI 34

3.4 | UWAZI KATIKA MASUALA YA ARDHI 37

3.5 | UWAZI KATIKA TASNIA YA UZIDUAJI 40

V | MCHAKATO: KUJITATHMINI 43

VI | MUKTADHA KITAIFA 45

VII | MAPENDEKEZO YA JUMLA 51

VIII | METHODOLOJIA NA VYANZO 53

IX | KIAMBATANISHO CHA MASHARTI UKUBALIFU 57

EXECUTIVE SUMMARY

INDEPENDENT REPORTING MECHANISM (IRM): TANZANIA PROGRESS REPORT 2014-2015

Tanzania's action plan boasts well-targeted commitments that, if implemented, will advance access to information, as well as improve public oversight of the extractive and land-management sectors. However, improving the level of civic participation in commitments needs greater emphasis, in addition to ensuring that implementation targets are met.

The Open Government Partnership (OGP) is a voluntary international initiative that aims to secure commitments from governments to their citizenry to promote transparency, empower citizens, fight corruption, and harness new technologies to strengthen governance. Tanzania began its formal participation in September 2011.

The State House Good Governance Coordination Unit, located in the Presidency, serves as the secretariat of OGP in Tanzania. Further support for implementation of commitments at city, municipal, and district level comes from the Prime Minister's Office for Regional Administration and Local Government.

A steering committee, made of government officials and civil society representatives oversees the implementation of the second action plan.

OGP PROCESS

Countries participating in the OGP follow a process for consultation during development of their OGP action plan and during implementation.

The government used the online OGP Portal to make the notice and format available for comments by the public on the draft action plan. With only 20 per cent of the Tanzanian population having access to the Internet, consultation may have been limited.

The government invited a variety of stakeholders for the consultation on the development of the action plan. Over 80 institutions and organizations were invited and took part in the consultative meeting held in Dar es Salaam. There was a lack of representation from trade unions - a key part of civil society in Tanzania - as well as a lack of private sector organizations. Parliamentarians were not involved in drafting the action plan. The mainstream media was well represented, including, for the first time, Tanzanian bloggers. Despite high participation in the meeting, few comments were ultimately accepted into the plan. Final decisions concerning the action plan's development and its implementation rested with the government OGP secretariat.

The government designated a steering committee to oversee the implementation of the second action plan. The committee met on ad hoc basis in Dar es Salaam. The committee has not published any progress reports. The self-assessment report was not published in 2015.

AT A GLANCE

MEMBER SINCE:	2011
NUMBER OF COMMITMENTS:	5
LEVEL OF COMPLETION:	
LIMITED:	4 of 5
NOT STARTED:	1 of 5
TIMING	
ON SCHEDULE:	0 of 5
COMMITMENT EMPHASIS:	
ACCESS TO INFORMATION:	5 of 5
CIVIC PARTICIPATION:	0 of 5
PUBLIC ACCOUNTABILITY:	2 of 5
TECH & INNOVATION FOR TRANSPARENCY & ACCOUNTABILITY:	3 of 5
NUMBER OF COMMITMENTS THAT WERE:	
CLEARLY RELEVANT TO AN OGP VALUE:	5 of 5
OF TRANSFORMATIVE POTENTIAL IMPACT:	1 of 5
SUBSTANTIAL OR COMPLETE IN IMPLEMENTATION:	0 of 5
ALL THREE (✪):	0 of 5

This report was prepared by Ngunga Greyson Tepani, an independent researcher

COMMITMENT IMPLEMENTATION

As part of OGP participation, countries make commitments in a two-year action plan. The Tanzanian action plan contains five commitments. The following tables summarise for each commitment the level of completion, potential impact, whether it falls within Tanzania's planned schedule and the key next steps for the commitment in future OGP action plans.

The IRM methodology includes starred commitments. These commitments are measurable, clearly relevant to OGP values as written, of transformative potential impact, and substantially or completely implemented. Tanzania's action plan contains no starred commitments. Note that the IRM updated the star criteria in early 2015 in order to raise the bar for model OGP commitments. In addition to the criteria listed above, the old criteria included commitments that have moderate potential impact. Under the old criteria, Tanzania would not have received any starred commitments. See http://www.opengovpartnership.org/node/5919 for more information.

Table 1 | Assessment of Progress by Commitment

COMMITMENT SHORT NAME	POTENTIAL IMPACT				LEVEL OF COMPLETION				TIMING
✪ COMMITMENT IS CLEARLY RELEVANT TO OGP VALUES AS WRITTEN, HAS TRANSFORMATIVE POTENTIAL IMPACT, AND IS SUBSTANTIALLY OR COMPLETELY IMPLEMENTED.	NONE	MINOR	MODERATE	TRANSFORMATIVE	NOT STARTED	LIMITED	SUBSTANTIAL	COMPLETE	
3.1. Access to information									Behind Schedule
3.2. Open data									Behind Schedule
3.2.1. Coordinating body									As Above
3.2.2. Data management									As Above
3.2.3. Review data disclosure policy									As Above
3.2.4. Open data policy									As Above
3.2.5. Open data portal									On Schedule
3.2.6. Key sets of open data on portal									As Above
3.3. Open budgets									Behind Schedule

COMMITMENT SHORT NAME	POTENTIAL IMPACT				LEVEL OF COMPLETION				TIMING
✪ COMMITMENT IS CLEARLY RELEVANT TO OGP VALUES AS WRITTEN, HAS TRANSFORMATIVE POTENTIAL IMPACT, AND IS SUBSTANTIALLY OR COMPLETELY IMPLEMENTED.	NONE	MINOR	MODERATE	TRANSFORMATIVE	NOT STARTED	LIMITED	SUBSTANTIAL	COMPLETE	
3.3.1. Yearly budget reports									As Above
3.3.2. Parliamentary Audit Committees reports									As Above
3.3.3. Monthly tax exemptions management									As Above
3.3.4. Machine-readable budget data									As Above
3.4. Land transparency									**As Above**
3.4.1. Demarcated areas									As Above
3.4.2. Land Use Plan									On time
3.4.3. Online land ownership database									As Above
3.5. Extractive industries transparency									**As Above**
3.5.1. Publish mining development agreements (MDAs) & Profit Sharing Contracts (PSCs) from 2014 onwards									As Above
3.5.2. Disclosure of contracts signed before 2014									As Above
3.5.3. Publish demarcated mining areas by December, 2015									As Above

Table 2 | Summary of Progress by Commitment

NAME OF COMMITMENT	SUMMARY OF RESULTS
3.1: Access to information • OGP value relevance: Clear • Potential impact: Transformative • Completion: Limited	This commitment aims to enact an Access to Information (ATI) law that was evolved from a commitment outlined but not implemented in the first action plan. This commitment was not completed in the period under review. If implemented, this commitment would have a transformative impact as the bill and resultant act could exponentially increase public access to government-held information. It is recommended that the government improve its efforts in engaging and consulting with all relevant stakeholders as a first step towards realizing the bigger goal of having ATI legislation in place.
3.2: Open data • OGP value relevance: Clear • Potential impact: Moderate • Completion: Limited	This commitment envisions the development of a framework on open data that includes the formulation of policies, the establishment of an oversight body, and publication of data in a new portal. Only one milestone has recorded full completion (3.2.5) and another shows substantial progress (3.2.6). Significant effort is still needed to ensure full implementation. A new framework on open data is a major step for enabling public access to information. The government needs to implement the incomplete milestones by the 31 March 2016 deadline. It is also recommended that the government designates and strengthens the capacity of one lead agency for data coordination purposes, as well as ensure mirroring of the data published in opendata.go.tz in each relevant ministry, department or agency website.
3.3: Open budgets • OGP Value Relevance: Clear • Potential Impact: Moderate • Completion: Limited	This commitment sets an ambitious goal to publish eight budget reports considered to meet the international criteria for budget transparency in machine-readable format. Although improvements have been made in the release of budget reports, two of eight key reports were not published, namely the mid-year review and the end-of-year budget reports. The published data is not available in real time or machine readable format. It is recommended that the role of publishing budget data and related information be coordinated through one agency, instead of being scattered amongst various ministries and departments.
3.4: Land transparency • OGP Value Relevance: Clear • Potential Impact: Moderate • Completion: Limited	This commitment seeks to ensure a fair and equitable governance of land matters through the publication of land use plans, ownership information, and demarcated areas. The government had committed to publish demarcated areas for large-scale agricultural investment (farming and livestock keeping) and to provide an online resource or database on land ownership in Tanzania that is easily searchable. This commitment has limited completion, as some of this data is not readily available as outlined in the action plan. It is recommended that the government ensures periodic and real time publication of land ownership data.
3.5: Extractive industries transparency • OGP Value Relevance: Clear • Potential Impact: Moderate • Completion: Not started	This commitment aims to fulfil Tanzania's Extractive Industries Transparency Initiative (EITI) commitments by June 2015. Tanzania, has been EITI compliant since 2012 but was suspended in September 2015 as a consequence of missing a deadline for the publication of the 2012–13 report by 30 June 2015. A year after the action plan implementation, no action has taken place on any of the milestones listed in the commitment.Although outside of the evaluation period, the suspension from the EITI was lifted on 17 December 2015 as a result of the required revenue report published on 27 November 2015. This commitment represents an important step to ensure effective and transparent management of extractive industries. It is recommended that the government publishes the government's policy on actual practice for disclosure of contracts, all signed mining development agreements, and profit-sharing contracts from 2014 onwards through offline and online means.

RECOMMENDATIONS

There remains a need for Tanzania to improve the quality and scope of dialogue during action plan development and implementation. This should include establishing a meaningful dialogue mechanism, using the existing web portal to communicate progress, publishing progress reports, and designating government points of contact for commitments. Existing commitments, such as the access to information law, budget information, and land ownership commitments, are well targeted and should be implemented with urgency. The action plan could include commitments targeted at disclosing public officials' assets and civic participation at the local government level. Based on the challenges and findings identified in this report, this section presents the principal recommendations.

TOP FIVE "SMART" RECOMMENDATIONS
1. **The consultation process during the development of the action plan needs to be more open.** The government could improve awareness-raising efforts by properly informing the public of the timeline, format and general process. All data made available for public use should be translated to Kiswahili to allow countrywide access to information.
2. **Establish a formal dialogue mechanism to allow monitoring of progress and ensure better accountability from implementing agencies.**
3. **Without further delay, the government should submit to parliament the draft of the access to information law** ensuring the following: (1) that a proper consultation is held, (2) that it is submitted on its own for parliament approval, and (3) that it complies with international standards.
4. **Prepare legislative amendments and regulations to strengthen asset disclosure of public officials.**
5. **The government should establish a user friendly interface to publish government data in accessible format, including developing proper feedback mechanisms to ensure the involvement of citizens at local government level.**

ELIGIBILITY REQUIREMENTS

To participate in OGP, governments must demonstrate commitment to open government by meeting minimum criteria on key dimensions of open government. Third-party indicators are used to determine country progress on each of the dimensions. For more information, see section IX: Eligibility Requirements at the end of this report or visit: http://www.opengovpartnership.org/how-it-works/eligibility-criteria.

Ngunga Greyson Tepani is an independent researcher.

OGP aims to secure concrete commitments from governments to promote transparency, empower citizens, fight corruption, and harness new technologies to strengthen governance. OGP's Independent Reporting Mechanism assesses development and implementation of national action plans in order to foster dialogue among stakeholders and improve accountability.

MUHTASARI

MPANGO TATHMINI WA TAARIFA (IRM): TANZANIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI 2014-2015

Mpango kazi wa Tanzania unajivunia maazimio yaliyoelekezwa vyema ambayo, kama yakitekelezwa, yataongeza upatikanaji wa taarifa, pia kuboresha usimamizi wa uendeshaji wa sekta za ardhi na tasnia ya uziduaji. Hata hivyo, uboreshaji wa namna watu na asasi za kiraia zinanavyoweza kushiriki katika utekelezaji wa maazimio unahitaji msisitizo zaidi, juu ya kuhakikisha kuwa malengo ya utekelezaji yanafikiwa.

Mpango wa Utendaji Kazi wa Serikali kwa Uwazi (OGP) ni juhudi za wadau kadhaa, wanaojitolea kimataifa kwa nia ya kupata maazimio mahsusi kutoka kwa serikali mbalimbali kwenda kwa wananchi wake ili kuhimiza uwazi, kuwawezesha wananchi, kupambana na rushwa, na kutumia teknolojia mpya kwa lengo la kuboresha utawala bora. Tanzania ilijiunga rasmi na Mpango wa OGP mnamo Septemba 2011.

Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora, kilichopo Ikulu ya Rais, ndio sekretarieti ya OGP nchini Tanzania. Pia, msaada wa utekelezaji wa maazimio hupatikana katika ngazi ya jiji, manispaa na wilaya kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI).

Kamati Elekezi, inayoundwa na wawakilishi kutoka serikalini na asasi za kiraia husimamia utekelezaji wa mpango kazi wa pili (wa OGP).

MCHAKATO WA OGP

Nchi zinazoshiriki katika mpango wa OGP zinafuata mchakato wa ushirikishaji wananchi wakati wa kuandaa mpango kazi na hata wakati wa utekelezaji wake.

Serikali ilitumia tovuti kuu yake ya OGP kuweka notisi na muundo wa kufikisha maoni kutoka kwa wananchi kutokana na rasimu ya mpango kazi. Lakini, kwa vile idadi ya Watanzania wenye uwezo wa kufikia huduma na intaneti ni asilimia ishirini tu, ushirikishwaji wa wananchi ulikuwa mdogo.

Serikali ilialika wadau mbalimbali ili kushauriana juu ya uandaaji wa mpango kazi. Zaidi ya taasisi themanini zilialikwa na kushiriki katika mkutano uliofanyika Dar es Salaam. Hakukuwa na uwakilishi kutoka vyama vya wafanyakazi – sehemu muhimu ya asasi za kiraia nchini – na taasisi za sekta binafsi.. Wabunge pia hawakushirikishwa katika kuandaa mpango kazi. Vyombo vikuu vya habari viliwakilishwa ipasavyo na kwa mara ya kwanza, mabloga wa Kitanzania walishirikishwa. Pamoja na ushiriki wa hali ya juu katika mkutano huo, ni maoni machache tu ndiyo yaliyokubaliwa kuingizwa kwenye mpango. Maamuzi ya mwisho juu ya kukamilisha uandaaji mpango kazi na utekelezaji wake ulisalia serikalini kwenye sekretarieti ya OGP.

Serikali iliunda Kamati Elekezi ya kusimamia utekelezaji wa mpango kazi wa pili. Kamati hiyo ilikutana Jijini Dar es Salaam. Kamati hiyo haikuchapisha taarifa zozote za utekelezaji wala taarifa ya mwaka ya serikali kujitathmini juu ya utekelezaji wa maazimio.

KWA UFUPI

MWANACHAMA TANGU:	2011
JUMLA YA MAAZIMIO:	5
KIWANGO CHA UTEKELEZAJI:	
KIDOGO:	4 KATI YA 5
BADO KUANZA:	1 KATI YA 5
WAKATI	
KWA WAKATI:	0 KATI YA 5
MAAZIMIO KWA MHIMIZO:	
UPATIKANAJI TAARIFA:	5 KATI YA 5
USHIRIKISHI WA WATU:	0 KATI YA5
UWAJIBIKAJI:	2 KATI YA 5
TEKNOLOJIA NA UBUNIFU KWA AJILI YA UWAZI NA UWAJIBIKAJIY:	3 KATI YA 5
IDADI YA MAAZIMIO AMBAYO:	
YALIKUWA YANAENDANA NA TUNU ZA OGP:	5 KATI YA 5
YANA UTASHI MKUBWA:	1 KATI YA 5
YAMETEKELEZWA KWA KIASI KIKUBWA AU KUKAMILIKA KABISA:	0 KATI YA 5
VIGEZO VYOTE VITATU (✪):	**0 KATI YA 5**

Taarifa hii imeandaliwa na Ngunga Greyson Tepani, mtafiti wa kujitegemea

UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO

Kama sehemu ya ushiriki wa OGP, nchi huweka maazimio katika mpango kazi wa miaka miwili. Mpango kazi wa Tanzania una maazimio matano. Majedwali yafuatayo yanatoa muhtasari wa kila azimio, kiwango cha utekelezaji kilichofikiwa, utashi uliomo na hatua muhimu za kufuatwa kwa azimio ndani ya mipango kazi ijayo ya OGP.

Methodolojia ya IRM inajumuisha maazimio nyota. Maazimio haya ni yale ambayo yanapimika, kwa jinsi yalivyoandikwa na yanaendana na tunu za OGP yenye kubadili mfumo au utashi mkubwa na kwamba yametekelezwa kwa kiasi kikubwa au kwa ukamilifu kabisa. Mpango kazi wa Tanzania haukuwa na maazimio nyota. Ikumbukwe kuwa MTTilibadilisha vigezo vya maazimio nyota mapema mwaka 2015 ili kupandisha kiwango cha modeli za maazimio ya OGP. Pamoja na vigezo vilivyotajwa hapo juu, vigezo vya zamani vilijumuisha maazimio yenye utashi wa kadiri/kati. Hata kwa kutumia vigezo vya zamani, Tanzania isingepata maazimio nyota. Kwa ufafanuzi zaidi tembelea (http://www.opengovpartnership.org/node/5919).

Jedwali la 1 | Tathmini ya utekelezaji kwa kila azimio

JINA LA AZIMIO KWA KIFUPI	ATHARI TARAJIWA				KIWANGO CHA UTEKELEZAJI				KWA WAKATI
✪ AZIMIO LINAPIMIKA, LINANENDANA NA TUNU ZA OGP, LENYE ATHARI CHANYA KWA JAMII AU UTASHI MKUBWA NA LIMETEKELEZWA KWA KIASI KIKUBWA AU LIMETEKELEZWA KIKAMILIFU.	HAKUNA	KIDOGO	WASTANI	MABADILIKO MAKUBWA	BADO KUANZA	KIASI KIDOGO	KIASI KIKUBWA	TIMILIFU	
3.1: Upatikanaji taarifa									Nyuma ya Wakati
3.2: Takwimu huria									Nyuma ya Wakati
3.2.1.Chombo cha uratibu									Nyuma ya Wakati
3.2.2. Usimamizi wa takwimu									Nyuma ya Wakati
3.2.3. Kupitia upya sera ya kuruhusu kuchapisha takwimu/data									Nyuma ya Wakati
3.2.4. Sera ya takwimu huria									Nyuma ya Wakati
3.2.5. Tovuti kuu ya takwimu huria									Kwa Wakati
3.2.6. Kuweka takwimu muhimu kwenye tovuti kuu									Kwa Wakati

JINA LA AZIMIO KWA KIFUPI	ATHARI TARAJIWA				KIWANGO CHA UTEKELEZAJI				KWA WAKATI
	HAKUNA	KIDOGO	WASTANI	MABADILIKO MAKUBWA	BADO KUANZA	KIASI KIDOGO	KIASI KIKUBWA	TIMILIFU	
3.3: Uwazi katika bajeti									**Nyuma ya Wakati**
3.3.1. Taarifa za bajeti za mwaka									Nyuma ya Wakati
3.3.2. Taarifa za Kamati ya Bunge ya Ukaguzi wa Fedha									Nyuma ya Wakati
3.3.3. Taarifa za usimamizi wa misamaha ya kodi ya kila mwezi									Nyuma ya Wakati
3.3.4. Takwimu / data za bajeti kuwekwa katika mfumo utakaowezesha takwimu hizo kusomwa na mashine									Nyuma ya Wakati
3.4: Uwazi katika masuala ya ardhi									**Nyuma ya Wakati**
3.4.1. Maeneo yaliyotengwa									Nyuma ya Wakati
3.4.2. Mpango wa matumizi ya ardhi									Nyuma ya Wakati
3.4.3. Kanzi ya takwimu kuhusu umiliki ardhi kuwekwa mtandaoni									Nyuma ya Wakati
3.5. Uwazi katika tasnia ya uziduaji									**Nyuma ya Wakati**
3.5.1. Chapisha mikataba ya uendelezaji madini (MDAs) & na mikataba ya mgawanyo wa faida (PSCs) tangu 2014 na kuendelea									Nyuma ya Wakati
3.5.2. Uwazi kwa mchakato wa mikataba iliyosainiwa kabla ya 2014									Nyuma ya Wakati
3.5.3. Chapisha maeneo yaliyotengwa kuchimba madini kufikia Desemba, 2015									Nyuma ya Wakati

Jedwali la 2 | Muhtasari wa utekelezaji kwa kila azimio

AZIMIO	RESUMEN
3.1: Upatikanaji wa taarifa • *Umuhimu kwa tunu tajwa ya OGP:* Wazi • *Athari tarajiwa:* Mabadiliko makubwa • *Utekelezaji:* Kiasi kidogo	Serikali ilidhamiria kupitia azimio hili, kutunga sheria ya upatikanaji wa taarifa kutoka serikalini (ATI), dhamira iliyotokana na azimio lililokuwemo, ingawa halikutekelezwa, kwenye mpango kazi wa kwanza wa OGP. Azimio hili halikutekelezwa kwa kipindi kinachofanyiwa tathmini ingawa serikali ilipeleka mswada huo wa ATI bungeni ambako haukupita. Kama azimio hili lingetekelezwa, lingeleta athari chanya kwakuwa sheria ingewawezesha, kwa kiasi kikubwa, wananchi kupata au kuzifikia taarifa za serikali. Wadau wametanabaisha kuwa mswada ulikuwa na mapungufu kwenye suala moja muhimu ambalo ni kutoshughulikia sheria zilizopo zinazokandamiza upatikanaji wa habari ikiwa ni pamoja na sheria za Magazeti na Huduma za Utangazaji. Inapendekezwa kuwa, serikali iboreshe juhudi zake za kuongea na kushauriana na wadau wote kama hatua ya kwanza ya kuwa na sheria ya upatikanaji wa taarifa za serikali (ATI).
3.2: Takwimu huria • *Umuhimu kwa tunu tajwa ya OGP:* Wazi • *Athari tarajiwa:* Wastani • *Utekelezaji:* Kiasi kidogo	Azimio hili linapendekeza mfumo wa uundaji wa takwimu huria unaojumuisha uandaaji wa sera, uanzishaji wa chombo cha usimamizi, na kuruhusu uchapishaji wa takwimu hizo katika tovuti kuu mpya. Hatua moja tu ya azimio hili ndio imekamilka kiutekelezaji (3.2.5) na nyingine inaonesha utekelezaji kwa kiasi kikubwa (3.2.6). Juhudi kubwa zinahitajika kuhakikisha kuwa azimio limekamilika. Mfumo mpya wa takwimu huria ni hatua muhimu ya wananchi kuzifikia na kupata taarifa. Inafaa kwa serikali kukamilisha utekelezaji wa hatua zilizosalia itakapofikia Machi 2016. Pia inashauriwa kuwa serikali itambue na kuipa uwezo wakala- kiongozi itakayoratibu shughuli za upatikanaji wa takwimu na kuhakikisha kuwa takwimu zilizochapishwa kwenye tovuti ya opendata.go.tz zinapatikana pia kwenye tovuti za wizara, idara na wakala husika.
3.3: Uwazi katika Bajeti • *Umuhimu kwa tunu tajwa ya OGP:* Wazi • *Athari tarajiwa:* Wastani • *Utekelezaji:* Kiasi kidogo	Azimio hili limeweka utashi mkubwa wa kuchapisha taarifa nane muhimu za bajeti ambazo zinaendana na vigezo vya kimataifa vya uwazi katika bajeti kwa mfumo utakaowezesha takwimu kusomwa na mashine. Pamoja na kuwa kuna maboresho katika utoaji wa taarifa za bajeti, taarifa mbili kati ya nane hazikuchapishwa. Taarifa hizo ni mapitio ya nusu mwaka ya bajeti na taarifa za mwaka za bajeti. Takwimu zilizochapishwa hazikutolewa kwa wakati au kwa mfumo unaowezesha takwimu kusomwa na mashine. Inapendekezwa kuwa jukumu la kuchapisha takwimu liwekwe kwa wakala mmoja, badala ya kutawanywa kati ya wizara na idara zingine za serikali zinazohusika na azimio tajwa.
3.4: Uwazi katika masuala ya Ardhi • *Umuhimu kwa tunu tajwa ya OGP:* Wazi • *Athari tarajiwa:* Wastani • *Utekelezaji:* Kiasi kidogo	Azimio hili linadhamiria kuhakikisha usawa na stahiki katika usimamizi wa masuala ya ardhi kwa kuchapisha mipango ya matumizi ya ardhi, taarifa za umiliki ardhi na maeneo yaliyotengwa. Serikali iliazimia kuchapisha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji mkubwa kwenye kilimo (kilimo na ufugaji) na kuweka kanzi ya takwimu mtandaoni inayoonesha umiliki wa ardhi nchini Tanzania. Azimio hili limetekelezwa kwa kiasi kidogo kwani baadhi ya takwimu hizi hazipatikani kama ilivyoazimiwa kwenye mpango kazi. Inapendekezwa kuwa kuwa serikali ihakikishe kunakuwa na uchapishaji wa takwimu za umiliki ardhimara kwa mara na kwa wakati.
3.5: Uwazi katika Tasnia ya Uziduaji • *Umuhimu kwa tunu tajwa ya OGP:* Wazi • *Athari tarajiwa:* Wastani • *Utekelezaji:* Bado kuanza	Ambayo ilikuwa tarehe ya mwisho ya utekelezaji. Hakuna hatua hata moja – kama ilivyoandikwa kwenye mpango kazi - iliyotekelezwa katika azimio hili. Kwahiyo mtafiti wa IRM anaona kuwa azimio hili halijaanza kutekelezwa. Ingawa ni nje ya muda wa tathmini hii, uanachama wa EITI ulirejewa tena mnamo tarehe 17 Desemba 2015 baada ya serikali kuchapisha taarifa zilizokuwa zinahitajika mnamo tarehe 27 Novemba 2015. Azimio hili linawakilisha hatua muhimu ya kuhakikisha usimamizi wa tasnia ya uziduaji kwa ufanisi na uwazi. Inapendekezwa kuwa serikali ichapishe sera ya namna mikataba ya kabla 2014 imekuwa ikiwekwa wazi. Pia, ichapishe mtandaoni na nje ya mtandao mikataba yote ya MDAs na PSCs kuanzia

MAPENDEKEZO

Bado kuna haja kwa serikali ya Tanzania kukuza ubora na wigo wa majadiliano wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mpango kazi. Juhudi hizi zijumuishe na kuanzisha mfumo wa majadiliano wenye tija, kutumia tovuti kuu iliyopo ili kujulisha utekelezaji ulipofikia, kuchapisha taarifa za utekelezaji, na kuweka wazi wahusika wa mawasiliano kwa kila azimio. Maazimio yaliyopo, kama vile upatikanaji wa taarifa, taarifa za bajeti na umiliki wa ardhi, ni maazimio yenye malengo mazuri na yanapaswa kutekelezwa kwa haraka. Mpango kazi ujao ujumuishe maazimio yanayolenga kutangaza mali za watumishi wa umma na ushiriki wa wananchi katika ngazi ya serikali za mitaa. Kwa kufuata changamoto na matokeo yaliyomo kwenye taarifa hii ya tathmini, yafuatayo ni mapendekezo makuu.

MAPENDEKEZO MAKUU MATANO
1. **Mchakato wa mashauriano wakati wa kuandaa mpango kazi ni lazima uwe wazi zaidi.** Serikali inaweza kuboresha juhudi za uelimishaji kwa kuihabarisha jamii juu ya wakati, mfumo na mchakato mzima. Taarifa au takwimu zote kwa matumizi ya wananchi lazima ziwekwe pia kwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wananchi walio wengi nchi nzima kuielewa.
2. **Kuanzisha mfumo rasmi wa majadiliano utakaowezesha usimamizi wa utekelezaji na kuhakikisha uwajibikaji kwa wakala zinazohusika na utekelezaji wa maazimio.**
3. **Bila ya kukawia, serikali ipeleke mswada bungeni wa sheria ya upatikanaji wa taarifa** ikizingatia yafuatayo: (a) kwamba majadiliano ya dhati yanafanyika, (b) kwamba inapelekwa bungeni ili bunge liridhie kuwa sheria, na (c) sheria hiyo iendane na sheria zingine za mfano kimataifa.
4. **Serikali iandae marekebisho ya sheria na kanuni ili kuimarisha dhamira ya kutangaza mali za watumishi wa umma.**
5. **Serikali ianzishe jukwaa la wazi ambamo wananchi/watumiaji wa takwimu za serikali wanaweza kuzipata kirahisi au kuwasiliana nao ikiwa ni pamoja na kuunda mifumo ya kupata mrejesho wa watumiaji takwimu ili kuwepo na ushiriki wa wananchi hata katika ngazi ya serikali za mitaa.**

MASHARTI YA USTAHIKI

Ili kushiriki kwenye mpango wa OGP, serikali lazima zionyeshe dhamira ya kweli ya utendaji kazi kwa uwazi ili kufikia vigezo vya chini kwa vipimo vikuu vya serikali iliyo wazi. Viashiria vya ngazi ya tatu vinatumika kuamua hatua iliyofikiwa na nchi husika kwa kila kipimo. Kwa maelezo zaidi, angalia Sehemu IX juu ya masharti ya ustahiki mwishoni mwa taarifa hii au tembelea tovuti http://www.opengovpartnership.org/how-it-works/eligibility-criteria.

Ngunga Greyson Tepani ni mtafiti wa kujitegemea

Mpango wa Utendaji Kazi wa Serikali kwa Uwazi (OGP) una lengo la kupata maazimio mahususi kutoka katika serikali mbalimbali yatakayohimiza uwazi, kuwezesha wananchi, kupambana na rushwa, na kutumia teknolojia mpya ili kuboresha utawala bora. Mfumo wa Tathmini wa Taarifa za OGP (IRM) unahakiki uundaji na utekelezaji wa mipango kazi ya nchi mbalimbali ili kukuza majadiliano kati ya wadau na kukuza uwajibikaji.

I | USHIRIKI KITAIFA KWENYE OGP

HISTORIA YA USHIRIKI WA OGP

Mpango wa Utendaji Kazi wa Serikali kwa Uwazi (OGP) ni juhudi za wadau kadhaa, wanaojitolea kimataifa kwa nia ya kupata maazimio mahususi kutoka katika serikali mbalimbali kwa wananchi wake yatakayohimiza uwazi, kuwezesha wananchi, kupambana na rushwa na kutumia teknolojia mpya ili kuboresha utawala bora.

Kufikia malengo haya, OGP hutengeneza jukwaa kimataifa ili kujadili na kupeana uzoefu miongoni mwa serikali, AzaKi na sekta binafsi wote wakichangia katika nia ya kuzifanya serikali zitoe huduma kwa wananchi wake kwa uwazi.

Tanzania ilianza kushiriki rasmi mpango huu mnamo Septemba 2011, ambapo Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitangaza nia ya nchi yake kushiriki.[1]

Ili kushiriki kwenye mpango wa OGP, serikali lazima zioneshe dhamira yao ya utendaji kazi kwa uwazi ili kufikia vigezo vya chini kwa vipimo vikuu vya serikali iliyo wazi ambavyo mwishowe vitaongeza mwitikio wa serikali, kukuza ushiriki wa wananchi na kupambana na rushwa. Viashiria huru vya ngazi ya tatu vinatumika kuamua hatua iliyofikiwa na nchi husika kwa kila kipimo. Kwa maelezo zaidi tazama sehemu ya VIII: Masharti ya Ustahiki.

Kama sehemu ya ushiriki wa OGP, nchi huweka maazimio katika mpango kazi wa miaka miwili. Mipango kazi lazima ioneshe maazimio ya serikali juu ya OGP, ambayo huongeza kiwango cha utendaji wa serikali kuwa cha juu kuliko kile kilichopo sasa. Maazimio haya yanaweza kuendeleza maboresho yanayoendelea au kuanzisha shughuli kwenye eneo jipya kabisa.

Tanzania iliandaa mpango kazi wake wa pili kuanzia mwezi Aprili 2014. Mpango kazi huo uliwasilishwa rasmi Juni 2014 na utekelezaji wake uanze Julai mosi 2014 na kuishia 30 Juni 2016. Taarifa hii ya tathmini inatazama kipindi cha Julai mosi 2014 hadi Juni 30 2015. Hadi taarifa hii inaandikwa (Januari 2016), serikali ilikuwa bado haijachapisha taarifa yake ya kujitathmini.

MUKTADHA KITAASISI

Mpango wa OGP hapa Tanzania unaongozwa na Kamati Elekezi ya wawakilishi kutoka wizara za serikali, asasi za kiraia (AzaKi) na ofisi ya uratibu wa mpango huo nchini. Kitengo cha Uratibu wa Utawala Bora – Ikulu (SHGGC) ndio kitovu cha mchakato wa OGP hapa nchini. Watekelezaji wengine ni pamoja na Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Katiba na Sheria, Wakala wa Mitandao ya Serikali, Wizara ya Maji, Wizara ya Afya na Huduma za Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWMTAMISEMI), hutoa ushirikiano na wakati mwingine kutekeleza baadhi ya maazimio ya OGP katika ngazi za wilaya, manispaa, miji, kata na vituo. Kwa mfano, kwenye azimio linalohusu uwazi wa bajeti (3.3.), OWMTAMISEMI inahusika kiutekelezaji, lakini kwenye azimio la takwimu au data huria (3.2), OWM-TAMISEMI ina jukumu la kutoa ushirikiano.

Nchini Tanzania, OGP inaheshimu Mkakati wa Kitaifa wa Utawala Bora (NFGG), ulioandaliwa mnamo mwaka 1999 kuasisi mfumo wa utawala bora nchini. Mkakati wa NFGG unatekelezwa kwa ubia na wadau mbalimbali kitaifa ili kufikia malengo ya utawala bora. Ubia huo unahusisha serikali kuu na ya mitaa, sekta binafsi, na asasi za kidini na AzaKi.

Katika taarifa yake ya awali, IRM iliarifu kuwa sekretarieti ya OGP haikuwa na wafanyakazi wala rasilimali fedha za kutosha wakati wa utekelezaji wa mpango kazi wa kwanza. Ushahidi uliokusanywa kwenye kipindi hiki cha tathmini unaonesha hali haijabadilika, ambapo Mratibu na msaidizi wake, ndio wafanyakazi pekee wanaoshughulika na masuala ya OGP katika kitengo cha SHGGC.

Ushahidi mwingine unatotokana na mahojiano yaliyofanywa na mtafiti na mapitio ya makabrasha mtandaoni[2] unapendekeza kuwa shughuli zilizopangwa kufanyika hazitafanikiwa kwani zinahitaji mtaji mkubwa kuzitekeleza, kama rasimu za bajeti zake zikizingatiwa. Kwa mfano, Wizara ya Maji peke yake inahitaji kiasi cha shilingi bilioni 1.226 au kiasi cha dola za Kimarekani

571,000 ili kutekeleza maazimio matatu — huku sehemu kubwa ya bajeti inayopendekezwa ikitokana na ufadhili wa wabia wa maendeleo.

Wakati wa uandaaji wa mpango kazi wa kwanza, timu na uongozi wa OGP ilifanya juhudi kadhaa za kujenga uelewa wa wananchi kwa kuzishirikisha AzaKi na sekta binafsi. Sharti la kuwa na muda wa kupokea maoni lilizingatiwa na kuwekwa mtandaoni. Hata hivyo, wakati wa uandaaji wa mpango kazi wa pili, michakato hiyo haikufuatwa, ukiondoa mkutano wa majadiliano uliofanyika mnamo Juni 2014.

MAELEZO KWA UFUPI YA METHODOLOJIA

IRM huingia ubia na watafiti wa kujitegemea wenye uzoefu katika kila nchi mshiriki wa OGP ili kutafiti, kuhariri na kuzisambaza/kuzitangaza taarifa hizi za tathmini. Nchini Tanzania, IRM imeingia ubia na Ngunga Greyson Tepani, Mkurugenzi Mtendaji wa Muungano wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali - *Tanzania Association of Non-Governmental Organisations* (TANGO). Ana shahada ya uzamili katika masuala ya Maendeleo ya Uchumi wa Jamii kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Hadi tulipokuwa tukiandika taarifa hii ya tathmini huru, serikali ilikuwa haijachapisha taarifa yake ya kujitathmini.

Pamoja na hayo, Bw. Tepani alikusanya maoni ya AzaKi na kuhoji maafisa wa serikali husika na wadau wengine. Wafanyakazi wa OGP na jopo la wataalamu ilipitia rasimu kadhaa za taarifa hii.

Taarifa hii inafuatia tathmini ya awali juu ya utekelezaji wa OGP nchini, "Taarifa ya Utekelezaji Tanzania 2012–13," ambayo iliangalia uundaji wa mpango kazi wa kwanza na utekelezaji wake kuanzia Julai mosi 2012 hadi Juni 30, 2013.

Ili kupata maoni ya wadau mbalimbali, Bw. Tepani aliandaa mkutano wa wadau uliofanyika Jijini Dar es Salaam. Mkutano huu ulifanyika kwa kutumia mfumo wa makundi. Pia, alifanya mahojiano ya ana kwa ana na kwa njia ya simu na maafisa wa serikali na wadau wengine. Watano kati ya maafisa 12 wa serikali walijitolea kufanya mahojiano na mtafiti huyo wa IRM kwa njia ya simu na barua pepe. Katika taarifa hii, kwa kuzingatia maombi ya baadhi ya wahojiwa, majina ya vyanzo vya utafiti yamehifadhiwa.

Muhtasari wa mkutano na wadau na maelezo ya ziada yamo kwenye Viambatanisho.

[1] Open Government Partnership. Introduction to OGP in Tanzania http://www.opengovpartnership.org/country/tanzania accessed on 22 September 2015
[2] United Republic of Tanzania. Final OGP Action Plan for Water Sector (2014) http://bit.ly/20n38Yw accessed on 20 September 2015

II | MCHAKATO: UANDAAJI WA MPANGO KAZI

Rasimu ya mpango kazi iliandaliwa na maafisa wa serikali, na ilikuwa ni matokeo ya kuzingatia kwa makini hatua iliyofikiwa kiutekelezaji na mafunzo yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa mpango kazi wa kwanza (2012–13). Hata hivyo, serikali haikufanya juhudi za kukuza weledi wakati wa uandaaji mpango mpya na mashauriano yaliishia kwa wadau waalikwa tu.

Nchi zinazoshiriki mpango wa OGP zinafuata mchakato wa mashauriano wakati wa kuandaa mpango kazi wao wa OGP. Kwa mujibu wa vifungu vya maamuzi vya OGP, nchi ni lazima:

- Ziweke wazi na kwa kina mchakato wa kupata maoni na ushauri kutoka kwa wananchi na kuweka muda wa kufanya hivyo ujulikane (angalau mtandaoni) kabla ya mashauriano yenyewe
- Zitafute ushauri kwa mapana na jamii kitaifa, ikiwa ni pamoja na AzaKi na sekta binafsi, kupata maoni mengi yenye mitazamo tofauti, na kuandaa muhtasari wa mashauriano na kuweka kwenye mtandao muhtasari huo pamoja na maoni ya maandishi ya mtu mmoja mmoja yaliyopokelewa
- Zifanye shughuli za kujenga weledi juu ya OGP ili kukuza ushiriki wa wananchi katika mashauriano
- Zishauriane na kutoa angalizo mapema kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na njia ya mtandao na mikutano ya ana kwa ana, na kuhakikisha kuwa fursa zinawafikia wananchi ili washiriki.

Sharti la tano, wakati wa mashauriano, limeainishwa kwenye Vifungu vya Maamuzi vya OGP. Sharti hili linatazamwa kwenye Sehemu ya III ya taarifa hii, Mashauriano wakati wa Utekelezaji:

- Nchi ziwe na jukwaa ambapo mashauriano ya mara kwa mara na wadau mbalimbali juu ya utekelezaji wa OGP yatafanyika. Jukwaa hili, laweza kuwa lilikuwepo au jipya.

Hili linashughulikiawa katika sehemu inayofuata, lakini ushahidi wa mashauriano kabla na baada ya utekelezaji umejumuishwa hapa kwenye Jedwali namba 1 kwa urahisi wa rejea.

Jedwali namba 1 | Mchakato wa mashauriano ya Mpango Kazi

AWAMU YA MPANGO KAZI	SHARTI LA MCHAKATO WA OGP (SEHEMU YA VIFUNGU VYA USIMAMIZI)	JE, SERIKALI ILITIMIZA SHARTI HILI?
Wakati wa kuandaa	Je, muda na mchakato ulifahamika kabla ya mashauriano?	Hapana
	Muda uliwekwa mtandaoni?	Hapana
	Je, muda ulipatikana kwa njia nyingine?	Hapana
	Onyesha kiungo (mtandaoni) kinachothibitisha muda ulitolewa.	HAIHUSIKI
	Je, kulikuwa na notisi kabla ya mashauriano?	Ndiyo

	Siku ngapi za notisi kabla ya mashauriano zilitolewa?	6
	Je, muda wa notisi hii ulitosha?	Hapana
	Je, serikali ilifanya shughuli zozote za kujenga weledi?	Hapana
	Onyesha kiungo (mtandaoni) -kinachothibitisha shughuli za kujenga weledi zilifanyika.	HAIHUSIKI
	Kulikuwa na mashauriano mtandaoni?	Hapana
	Kulikuwa na mashauriano ya ana-kwa-ana?	Ndiyo
	Je, muhtsari wa maoni ya washiriki ulipatikana?	Hapana
	Mashauriano hayo yalikuwa wazi mtu yeyote kushiriki au kwa kualikwa tu?	Kwa kualikwa tu
	Weka mashauriano kwenye spektra ya IAP2.[1]	Shauriana
Durante la implementación	Je, kulikuwepo na jukwaa la mara kwa mara la mashauriano wakati wa utekelezaji mpango?	Ndiyo
	Mashauriano hayo yalikuwa wazi mtu yeyote kushiriki au kwa kualikwa tu?	Kwa kualikwa tu
	Weka mashauriano kwenye spektra ya IAP2.	Shauriana

NOTISI KABLA YA MASHAURIANO NA KUJENGA WELEDI

Ukilinganisha na mpango kazi wa kwanza wa OGP, haikufahamika mara moja kupitia mahoajiano ya IRM na mkutano wa wadau kama serikali ilifanya shughuli zozote za kujenga weledi kabla ya kuandaa mpango kazi wa pili wa OGP. Hakuna ushahidi wowote unaoonyesha kulikuwapo na juhudi zilizofanywa na serilkali za kuelimisha umma.

Pamoja na hayo, serikali ilitumia lando la mtandao wa OGP nchini (http://www.opengov.go.tz) kuiweka notisi na muundo wa utoaji maoni kwa wananchi kwa rasimu ya mpango kazi. Tatizo ni kuwa, ni asilimia 20 tu ya idadi ya watu nchini Tanzania ndio wanafikiwa na huduma za intaneti[2].

Kwa kiasi kikubwa, notisi na mialiko kwa wadau ilitumwa kwa nakala halisi kwa washiriki watarajiwa wote. Notisi haikuwa na tarehe[3] kitu kilichofanya kuwa vigumu kupima utoshelevu wake.

UBORA NA WIGO WA MASHAURIANO

Serikali ya Tanzania ilifanya juhudi za kuwaalika wadau wengi na tofauti tofauti, wakati wa kuandaa mpango kazi wa pili wa OGP. Zaidi ya taasisi na asasi 80 zilialikwa na kushiriki wakati wa mkutano wa kuandaa mpango kazi. Washiriki 60 kati ya hao walikuwa ni wawakilishi wa AzaKi.[4] Kupitia mahojiano, mtafiti wa

IRM aliarifiwa kuwa maoni pia, yaliombwa kwa njia ya barua pepe kwenda AzaKi kadhaa. Hata hivyo, sekretarieti ya OGP ilipoombwa kutoa nakala ya barua pepe zilizorudi kwao au hata picha inayoakisi maoni yaliyopokelewa, haikuweza kufanya hivyo. Mkutano na wadau mbalimbali ulifanyika mahali ambapo waalikwa tu ndio walioweza kushiriki.

AzaKi na wadau nje ya seriali waliokuwepo kwenye mkutano huo ni pamoja na:

- Chuo Kikuu cha Mzumbe
- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
- Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)
- Asasi ya Twaweza
- *Economic and Social Research Foundation (ESRF)*
- Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA)
- Kamisheni ya Huduma za Jamii ya Kikristo (CSSC)
- Baraza la Habari Tanzania
- *The Leadership Forum*

Kama ilivyokuwa kwenye uandaaji wa mpango kazi wa kwanza (2012–13), hakukuwa na uwakilishi wa vyama vya wafanyakazi, ambavyo ni sehemu muhimu ya jamii ya kiraia hapa Tanzania, wala asasi za sekta binafsi. Mbali na washiriki waliotajwa hapo juu, vyombo vikuu vya habari hapa nchini viliwakilishwa vyema kwenye mkutano huo wa mashauriano, ikiwa ni pamoja na mabloga ambao walihudhuria kwa mara ya kwanza..

Pamoja na kwamba jamii ya kiraia ilishiriki kama sehemu ya Kamati Elekezi ya OGP (wakati wa kuandaa rasimu ya mpango kazi) uamuzi wa mwisho juu ya uandaaji na utekelezaji wa mpango kazi umekuwa ni wa sekretarieti ya OGP. Kutokana na mahojiano[5] na maoni mtandaoni[6], mkutano wa mashauriano ulikuwa shirikishi na washiriki walikuwa huru kutoa maoni. Ingawa mshiriki mmoja aliona kuwa uamuzi wa mwisho ni wa wale wenye mpango (serikali) na kuwa washiriki hawakuwa na nguvu ya kubadili kwa kiasi kikubwa kile kilichoazimiwa/kinachoazimiwa. Pamoja na hayo, mshiriki huyo alikiri kuwa baadhi ya maoni yao yalijumuishwa kwenye hatua mpya za maazimio.

Mkutano huo wa anakwaana ulifanyika Dar es Salaam, na kutokana na changamoto za kifedha zilizokuwa zikiikumba sekretarieti ya OGP[7], kulikuwa na uwakilishi finyu mno kutoka kwenye maeneo menigine ya kijiografia nchini. Serikali haikuwashirikisha wabunge hata wale waliokuwa wakipaza sauti kuhusu baadhi ya masuala ya mpango kazi wa kwanza. Hii ni fursa iliyopotea huku serikali ikidai ukosefu wa rasilimali ambazo zingewezesha kupanua wigo wa mashauriano, na mchakato wa kuunda Katiba Mpya kitaifa kama vikwazo-sababishi.

Hakukuwa na muhtsari wa maoni ya mkutano wa ana-kwa-ana wa mashauriano uliofanyika Juni 9, 2014 Jijini Dar es Salaam.

IRM iliarifiwa kuwa uandaaji wa mpango kazi umepitia tafsiri mbili kabla ya kupitishwa. Serikali ilionyesha maeneo muhimu kuzingatiwa, ambayo ni pamoja na maoni ya wasiriki wa mkutano wa ana-kwa-ana uliofanyika Jijini Dar es Salaam mnamo Juni 2014. Kwa bahati mbaya, nakala ya rasimu ya mpango kazi ukiwa na maoni ya washiriki haukutolewa kwa mtafiti wa IRM.

Fomu ya kupokea maoni wakati wa kuandaa mpango kazi ilitengenezwa na kutumwa kwa baadhi ya wadau; hata hivyo, mtafiti wa IRM hakuweza kuhakiki barua pepe zilizotumwa au maoni yaliyotolewa. Juhudi kadhaa za mtafiti wa IRM kuomba kupata maoni hayo na taarifa nyingine muhimu juu ya muundo wa OGP nchini Tanzania yaligonga mwamba.[8]

[1] "IAP2 Spektra ya Ushiriki Kisiasa", International Association for Public Participation, http://bit.ly/1kMmlYC
[2] Imetoka kwenye makala http://bit.ly/1L1EUqn
[3] Notice for public comment available on http://www.opengov.go.tz
[4] List of organisations and agencies involved in the development of the action plan.doc (2014). Makabrasha yaliyotumwa kwa barua pepe kwa mtafiti wa IRM mnamo tarehe 5 Septemba 2014
[5] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 6 September 2014
[6] Ben Taylor. http://bit.ly/1SWaOMD
[7] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 6 September 2014
[8] Barua pepe za mtafiti wa IRM zinazoomba taarifa tajwa 31 Agosti 2014 na kukumbushia tena 5 Sept 2014; 4 Jul 2015; 3 Sept 2015; 10 Desemba 2015 na 5 Jan 2016

III | UTEKELEZAJI WA MPANGO KAZI

Tanzania iliunda Kamati Elekezi ili kusimamia utekelezaji wa maazimio ya OGP kama yalivyoelekezwa kwenye mpango kazi wa pili. Jukumu la kamati hiyo lilikuwa ni kupima maendeleo ya utekelezaji na kuchukua hatua stahiki ili kufikia maazimio. Kamati elekezi hiyo ilikutana mara kadhaa Jijini Dar es Salaam, ambako wajumbe wengi na sekretarieti ya OGP wanapatikana.

MASHAURIANO YA MARA KWA MARA NA WADAU

Mtafiti wa IRM alikuwa amependekeza kuitisha mikutano ya kamati elekezi kwa kila robo mwaka ili kupunguza mzigo wa taasisi viongozi na kuwezesha taarifa za utekelezaji kupatikana kirahisi zaidi kila robo mwaka.

Mratibu wa OGP hakutoa orodha rasmi ya wajumbe wa kamati elekezi ya OGP kwa mtafiti wa IRM licha ya maombi kadhaa kwa njia ya barua pepe.[1] Kupitia mahojiano, mtafiti wa IRM alithibitisha kuwa ni AzaKi mbili tu, Twaweza na Chama cha Wanasheria Tanzania Bara (TLS) ndio walikuwa sehemu ya kamati elekezi ya OGP. Ilifahamika pia kwamba hili lilikuwa ni jukwaa lililofungwa kiushiriki, likiruhusu ushiriki wa maafisa wa serikali walioteuliwa na baadhi ya AzaKi. Baadhi ya nakala ya orodha ikionesha washiriki wengi wao wakiwa wawakilishi wa wizara, idara na wakala wa serikali zilitumwa kwa mtafiti wa IRM, lakini zilikuwa orodha zikionesha mikutano kadhaa maalumu iliyofanyika. Ni watano kati ya maafisa kumi na mbili wa serikali ndio waliokuwa tayari kufanyiwa mahojiano.

Kupitia mahojiano,[2] mtafiti wa IRM aligundua kuwa kulikuwa na changamoto za kufanya mikutano ya mara kwa mara iliyoratibiwa, ikiwa ni pamoja na wajumbe wengi kushindwa kuhudhuria vikao/mikutano.

Baadhi ya AzaKi ambazo hazikuweza kushiriki hata mkutano mmoja zilitoa sababu ya kutokufanya hivyo ni kukosekana kwa ajenda ya kupima maendeleo ya utekelezaji wa maazimio ya OGP kwenye vikao hivyo.[3] Ushahidi zaidi uliopatikana na mtafiti wa IRM unaonesha kuwa kwa baadhi ya vikao ya kamati washiriki walikuwa wanatoka taasisi moja tu — Ikulu.

Kwa mujibu wa mhojiwa mmoja,[4] vikao vingi vilivyofanyika vilikuwa ni kwa ajili ya maandalizi ya makongamano makubwa mawili ya OGP yaliyoandaliwa na serikali ya Tanzania: ambayo ni, Kongamano la OGP kwa kanda ya Afrika lililofanyika Mei 2015, na lile la Takwimu Huria kanda ya Afrika lililofanyika Septemba 2015.

Hadi taarifa hii inapoandikwa (Januari 2016), kamati elekezi imeshindwa kuwa na ufanisi katika kusimamia utekelezaji wa maazimio ya OGP na haikuchapisha taarifa yake ya kujitathmini ya kila mwaka. Lango la mtandao wa OGP halina taarifa za utekelezaji zaidi ya ile ya robo mwaka iliyochapishwa hivi karibuni ya utekelezaji wa OGP katika sekta ya maji.

[1] Barua pepe za mtafiti wa IRM zinazoomba taarifa tajwa 31 Agosti 2014 na kukumbushia tena 5 Sept 2014; 4 Jul 2015; 3 Sept 2015; 10 Desemba 2015 na 5 Jan 2016
[2] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 6 September 2014
[3] Anonymous. Telephone interviews with IRM researcher. 20 August 2015
[4] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 21 October 2015

IV | UCHAMBUZI WA YALIYOMO KWENYE MPANGO KAZI

Kila serikali inayoshiriki kwenye mpango huu wa OGP ni lazima iandae mpango kazi ambao una maazimio maalum kwa kipindi cha kuanzia cha miaka miwili. Serikali huandaa mipango kazi kwa kubainisha juhudi zilizopo sasa kuhusiana na uwazi wa utendaji serikalini, ikiwa ni pamoja na mikakati maalumu na programu zinazoendelea. Kisha mipango kazi huweka maazimio ya serikali ili kutekeleza OGP nchini, ambayo huenda mbali zaidi ya utendaji uliozoeleka serikalini. Maazimio haya yaweza kuboresha juhudi zilizopo kiutekelezaji zilipofikia kwa sasa, kutambua hatua mpya za kumalizia maboresho yanayoendelea kufanyika, au kuchukua hatua katika eneo jipya kabisa.

Maazimio ni lazima yaendane na upekee wa mazingira ya kila nchi na vipaumbele vya kisera. Maazimio ya OGP ni lazima yaendane na tunu za OGP kama zilivyotanabahishwa katika vifungu vya usimamizi wa OGP na Azimio la kuendesha serikali kwa uwazi lililosainiwa na serikali zote zinazoshiriki mpango wa OGP. Mfumo wa tathmini wa OGP (IRM) unatumia mwongozo ufuatao ili kupima uhusiano wa tunu za msingi za utendaji wa serikali kwa uwazi:

UPATIKANAJI TAARIFA

Maazimio haya:

- Yanahusu taarifa zinazoshikiliwa na serikali na sio taarifa za shughuli za serikali tu. Kwa mfano, kuchapisha au kutoa taarifa za uchafuzi mazingira ingekuwa na uhusiano hasa, ingawa taarifa hiyo haihusu"shughuli ya serikali" tu.
- Hayaishii kwenye takwimu au data tu ila ni kwa kila aina ya taarifa. Kwa mfano, kuweka wazi mikataba ya ujenzi mmojammoja na kiwango kikubwa cha takwimu za mikataba ya ujenzi.
- Yaweza kujumuisha uwekaji wazi wa taarifa katika mfumo wa takwimu au data huria na mifumo inayoruhusu jamii kuwekewa wazi takwimu au data.
- Yaweza kuhusu utoaji wa taarifa kabla hazijaombwa na/au baada ya kuombwa.
- Yaweza kuhusu wepesi wa upatikanaji wa takwimu na/au kuboresha usomekaji kiteknolojia wa takwimu;
- Yaweza kuhusu mifumo ya kuimarisha haki ya kupata taarifa (kama vile ofisi ya Mchunguzi Mkuu au mahakama za upatikanaji wa taarifa);
- Ni lazima yawezeshe ufikiwaji usio vikwazo wa taarifa (isiwe ni kwa upendeleo au matumizi ndani ya serikali tu);
- Yahamasishe uwazi wa michakato ya utoaji wa maamuzi ya serikali na utendaji kazi wake;
- Yanaweza kupigania upunguzaji gharama za kupata taarifa;
- Yahimize kufikia kiwango cha nyota 5 za kielelezo cha Takwimu/Data Huria (http://5stardata.info/).

USHIRIKI WA WANANCHI

Maazimio yanayohusu ushiriki wa wananchi yanaweza kuwa ushiriki rasmi hadharani au ushiriki mpana zaidi wa jamii. Kwa ujumla maazimio yajikite katika "ushauri," "ushirikishaji," "ushirikiano," au "uwezeshwaji," kama ilivyoelezwa katika Spektra ya Ushiriki wa Jamii ya Asasi ya Kimataifa inayoshughulikia Ushiriki wa Jamii (http://bit.ly/1kMmlYC).

Maazimio yanayoshughulikia ushiriki wa wananchi:

- Yafungue suala la utoaji maamuzi kwa wananchi wote watakaopenda; majukwaa haya mara nyingi ni maagizo "kutoka juu kwenda chini" kwani huundwa na serikali (au watendaji waliowezeshwa na serikali) ili kufikia maamuzi kwenye mduara wa sera;
- Mara nyingi huwa na vionjo vya upatikanaji wa taarifa ili kuwa na maoni yanayofaa kwa wananchi watakaopenda kuwa sehemu ya utoaji maamuzi;
- Mara nyingi yahusu kuboresha haki ya mwananchi ya kusikilizwa, ingawa sio haki ya kutekeleza kilichosemwa na mwananchi huyo.

Vinginevyo, maazimio yanaweza kuwa juu ya kuweka wigo mpana wa mazingira wezeshi kwa wananchi kushiriki. Mifano ni pamoja na:

- Maboresho yatakayokuza uhuru wa kujumuika, kujieleza, kulalamika au kupinga, habari, au kuunda vikundi/jumuiya;
- Maboresho juu ya vikundi/jumuiya ikiwemo sheria za vyama vya wafanyakazi au za asasi zisizokuwa za kiserikali (AZISE); na
- Maboresho yatakayokuza uwazi na michakato yenye kuthamini demokrasia kama vile maoni ya wananchi, uchaguzi, au maombi au mapingamizi.

Maazimio yafuatayo ni mfano wa maazimio ambayo yasingeweza kuendana na tafsiri pana ya neno, ushiriki wa wananchi:

- Maazimio ambayo yanachukulia kuwa ushiriki uta-ongezeka kwa kuchapisha taarifa bila ya kuelezea mfumo wa kushiriki ukoje (ingawa azimio kama hili lingechukuliwa kuwa ni la "upatikanaji taarifa");
- Maazimio ya ugatuzi ambayo hayaweki wazi mfumo mahsusi utakaokuza ushiriki wa jamii; na
- Maazimio yanayofasiri ushiriki kama ushirikiano baina ya taasisi kadhaa bila ya mfumo wa ushiriki wa jamii.

Maazimio ambayo yataonekana kuwa "hayana uhusiano ulio wazi" yanajumuisha pia mifumo ambamo ushiriki ni kwa taasisi au asasi zilizochaguliwa na serikali tu.

UWAJIBIKAJI

Maazimio ya kukuza uwajibikaji yanaweza kuhusu:

- Sheria, kanuni, na mifumo iliyowekwa inayowataka watendaji serikalini kuhalalisha matendo/maamuzi yao, kushughulikia kile wanachokosolewa au mahitaji yanayofikishwa kwao, na kuwajibika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria au maazimio.

Kama sehemu ya kuwa "serikali inayofanya kazi kwa uwazi", maazimio hayo lazima yawe na vionjo vya "uwazi", ikimaanisha sio mifumo tu ya uwajibikaji ndani ya serikali ilhali hakuna sura ya uwajibikaji kwa umma. Wakati ambapo maazimio hayo yanaweza kusifiwa na yanaweza kujibu changamoto kuu mojawapo ya OGP, hayawezi, kama yalivyowekwa, kupita kwenye kigezo cha "uhusiano ulio wazi" kwa kukosa uwazi. Pale ambapo mifumo hiyo inayoangalia ndani tu ni sehemu kuu ya mkakati wa serikali, inashauriwa kuwa serikali zijumuishe jukwaa la kuwasiliana na umma kama vile:

- Kuweka wazi taarifa kuu zisizo nyeti juu ya shughuli za taasisi (kwa kutumia utaratibu wa kuweka wazi kila kitu);
- Wanachi kuhakiki utendaji wa serikali; na
- Michakato ya rufaa inayoanzishwa na wananchi pale kunapokuwa hakuna utendaji au kuna ukiukwaji.

Maazimio imara kuhusiana na uwajibikaji yanahusu haki, wajibu, au matokeo ya hatua zilizochukuliwa na maafisa au taasisi. Maazimio rasmi ya uwajibikaji yanajumuisha namna ya kueleza/kufikisha kero au kutoa taarifa juu ya makosa na kupata majibu au fidia. Mifano ya maazimio imara ni pamoja na:

- Kuboresha au kuanzisha michakato ya ukataji rufaa pale serikali inapokataa kutoa taarifa;
- Kuboresha upatikanaji wa haki kwa kuweka mifumo ya utoaji haki nafuu, haraka, au rahisi zaidi kutumia;
- Kuboresha namna jamii itakavyoweza kuchunguza mifumo ya utoaji haki; na
- Kuanzisha mifumo ya kufuatilia michakato inayo-husu malalamiko ya wananchi (kama vile programu ya kompyuta inayowawezesha polisi kufuatilia kesi na kujua zimefikia hatua gani au namba za simu za kupiga bure kuripoti matukio ya rushwa).

Azimio ambalo linadai kuboresha uwajibikaji, lakini likidhani kwa kutoa taarifa au takwimu bila kuelezea namna au nini kifanyike ili taarifa isaidie kuleta matokeo au mabadiliko, halitachukuliwa kama ni azimio la uwajibikaji. Kwa maelezo zaidi tazama http://bit.ly/1oWPXdl.

TEKNOLOJIA NA UBUNIFU KWA UWAZI NA UWAJIBIKAJI

OGP ina lengo la kuongeza matumizi ya teknolojia na ubunifu ili kuiwezesha jamii kushiriki katika uendeshaji wa serikali. Hususani, maazimio yanayotumia teknolojia na ubunifu lazima yakuze uwazi na uwajibikaji kwa:

- Kukuza teknolojia mpya zinazotoa fursa ya kubadil-ishana taarifa, ushiriki wa wananchi, na ushirikiano.
- Kuweka taarifa nyingi zaidi wazi kwa wananchi ili waelewe jinsi serikali yao inavyofanya kazi na pia kuzishawishi serikali hizo katika utoaji wa uamuzi.
- Kupunguza gharama za kutumia teknolojia hizi kwa wananchi.

Zaidi, maazimio ambayo yatafikiriwa kuwa ya teknolojia na ubunifu:

- Yanaweza kujifunga kwenye mchakato wa kuzishirikisha AzaKi na wafanyabiashara kutambua utendaji wenye tija na njia zenye ubunifu kwa kutumia teknolojia mpya ili kuwapa mamlaka wananchi na kuhamasisha uwazi serikalini;
- Yanaweza kuunga mkono uwezo wa serikali na wananchi kutumia teknolojia kujenga uwazi na uwajibikaji;
- Yanaweza kuunga mkono matumizi ya teknolojia kwa watumishi wa serikali na pia wananchi.

Si kila marekebisho ya huduma za serikali mtandaoni yanaboresha uwazi wa serikali, pale azimio la huduma za serikali kimtandao linapowekwa,ni lazima lioneshe linakuza mojawapo ya yafuatayo: upatikanaji wa taarifa, ushiriki wa wananchi, au uwajibikaji kwa jamii.

VIGEZO MUHIMU

Zikitambua kuwa kutimiza maazimio ya utendaji wa serikali kwa uwazi kunashirikisha michakato inayochukua miaka, serikali haina budi kuweka muda na misingi kwa maazimio yao ambayo yanaonesha kipi kitatekelezwa kila mwaka, kwa kadiri inavyowezekana. Taarifa hii inaarifu kwa undani kila azimio ambalo Tanzania ililijumuisha kwenye mpango kazi wake, na kuyachambua maazimio kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji.

Wakati ambapo vigezo vilivyotumika kupima kila azimio vinajieleza wazi, baadhi vinahitaji maelezo ya ziada.

1. **Umahsusi:** Mtafiti wa IRM kwanza hupima kiwango cha umahsusi na kupimika kwa namna ambavyo kila azimio au hatua iliandikwa. Uchaguzi ni kati ya umahsusi/upimikaji:
    - Uko juu (maelezo ya azimio yako wazi, linapimika na kuna hatua zinazothibitishika ili kufikia lengo)
    - Wastani (maelezo ya azimio yako wazi, linapimika na ila hakuna hatua zinazothibitishika ili kufikia lengo)
    - Mdogo (azimio linaelezea shughuli ambayo inaweza kumaanisha kuwa inapimika lakini kupitia tasfiri binafsi ya msomaji)
    - Hakuna (azimio halina matokeo au hatua zinazoweza kuthibitika)
2. **Uhusiano:** Mtafiti wa IRM alipima kila azimio kuangalia uhusiano wake na tunu na changamoto kuu za OGP.
    - *Tunu za OGP:* Baadhi ya maazimio ya OGP hayako wazi ukitazama uhusiano wake na tunu za OGP. Ili kugundua visa vya namna hiyo, mtafiti wa IRM alifanya uamuzi kwa kusoma maneno yaliyomo kwenye azimio kwa umakini. Zoezi hili linafanya utambuzi wa maazimio ambayo yanaweka wazi zaidi uhusiano uliopo kati yao na masuala ya kimsingi kuhusiana na uwazi.
3. **Utashi:** Mtafiti wa IRM pia aliangalia utashi wa kila azimio, bila ya kuhukumu, endapo azimio lilitokana na juhudi mpya au zilizotangulia kabla ya uundaji wa mpango kazi ambazo zinatekeleza utendaji wa serikali juu zaidi ya ilivyozoeleka.
    - Ili kuchangia kwenye tafsiri pana ya utashi, mtafiti wa IRM aliangalia ni kwa kiasi gani azimio litabadilisha hatma ya eneo-sera husika. Hii itatokana na matokeo ya utafiti na uzoefu alionao mtafiti wa IRM kama mtaalamu wa sera. Ili kupima utashi tarajali, mtafiti wa IRM hutambua tatizo la kisera, kiwango cha msingi cha utendaji tangu mwanzo wa mpango kazi na kupima kiasi ambacho azimio, kama likitekelezwa, litaathiri utendaji na kudhibiti tatizo hilo la kisera.

Viashiria vyote na njia iliyotumika katika utafiti huu wa IRM vinapatikana katika Mwongozo wa Utaratibu wa IRM, unaopatikana kwenye tovuti ifuatayo: (http://www.opengovpartnership.org/about/about-irm).

Mwisho, kiashiria kimoja kina umuhimu wa pekee kwa wasomaji na kinasaidia kuongeza kasi baina ya nchi zinazoshiriki mpango wa OGP: maazimio nyota. Maazimio nyota ni yale yanayofikiriwa kuwa ya mfano kwa OGP. Ili kupata nyota, azimio lazima likidhi vigezo kadhaa kama ifuatavyo:

1. Lazima liwe la kipekee sana ambapo uamuzi juu ya utashi tarajali wake unaweza kufanywa. Maazimio nyota yatakuwa na umahsusi wa wastani au juu.

2. Lugha iliyotumika kwenye azimio ni lazima ioneshe wazi uhusiano wake na kuifanya serikali iwe inayotenda kazi kwa uwazi zaidi. Lazima kuwe na uhusiano wa kipekee na angalau moja ya tunu za OGP za upatikanaji wa taarifa, ushiriki wa wananchi au uwajibikaji kwa jamii.
3. Azimio litaleta athari kubwa inayotarajaliwa endapo litatekelezwa kikamilifu.
4. Mwisho, azimio ni lazima litekelezwe kwa kiasi kikubwa au kwisha kabisa kwa wakati uliopngwa kutekelezwa kwa mpango kazi.

Kwa kuzingatia vigezo hivi, mpango kazi wa Tanzania haukuwa na maazimio nyota.

IRM ilibadilisha vigezo vya maazimio nyota mapema mwaka 2015 ili kupandisha kiwango cha maazimio mifano ya OGP. Chini ya vigezo vya zamani, azimio lilichukuliwa kuwa ni nyota endapo linapimika, linaendana na tunu za OGP, lenye kubadili mfumo au utashi mkubwa na kwamba linatekelezeka kwa kiasi kikubwa au kwa ukamilifu kabisa. Hata kwa kutumia vigezo vya zamani, Tanzania isingepata maazimio nyota.

Mwisho, grafu zilizomo kwenye sehemu hii zinaonyesha muhtasari tu wa utajiri wa takwimu zinazokusanywa na IRM wakati wa mchakato wa kuandaa taarifa ya utekelezaji. Kwa takwimu zote za Tanzania, na nchi nyingine zinazoshiriki mpango wa OGP, tazama *OGP Explorer*[1].

MAELEZO YA JUMLA YA MAAZIMIO

Kwa ujumla, mpango wa pili wa Tanzania wa OGP (2014–16) ulikuwa ni hatua kubwa ikilinganishwa na mpango wa kwanza (2012–13), ukiwa na idadi ya maazimio ya kutekeleza kiuhalisia na kuweka wazi zaidi viashiria na muda maalumu wa kufikiwa kwa maazimio hayo. Ikilinganishwa na maazimio 25 yaliyokuwa yatekelezwe ndani ya kipindi cha mwaka mmoja katika mpango wa kwanza, serikali ilichagua kuwa na maazimio matano tu kwa kipindi cha miaka miwili katika mpango wa pili. Pia mchakato wa uundaji mpango mara hii uliboreka kwani ulijumuisha wadau wengi, ingawa haukuwa wazi vya kutosha.

Mpango wa pili umejikita kwenye kuwapatia wananchi taarifa zinazoshikiliwa na serikali na kuboresha uwazi katika mgawanyo wa matumizi ya ardhi na tasnia ya udukuzi. Mpango unajumuisha maeneo mahususi ya kipaumbele matano ambayo ni: (1) upatikanaji wa taarifa, (2) uwazi katika bajeti, (3) uwazi wa takwimu au data huria, (4) uwazi katika sekta ya ardhi, na (5) uwazi katika tasnia ya udukuzi. Mpango unaonesha ni kitengo gani cha serikali kinaongoza au kusaidia katika utekelezaji wa kila azimio. Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwenye mpango wa kwanza, hakukuwapo na watu wa kuwasiliana kwa kila azimio. Mtafiti wa IRM baada ya kuomba, alipewa orodha ya maafisa wa serikali kuwasiliana nao kwa vile haikuwa inajulikana kabla kwa umma. Serikali haikuchapisha taarifa za kujitathmini za robo mwaka wala ya mwaka mtandaoni kama ilivyotakiwa kufanya.

3.1 | UPATIKANAJI WA TAARIFA

Maelezo kamili ya azimio:

Kutunga Sheria ya upatikanaji wa taarifa hadi itakapofika Desemba mwaka 2014.

Sheria itatungwa kwa kuzigatia mifano bora kimataifa na itajumuisha:

(i) Kutambua uwepo wa haki ya kupata taarifa, pamoja na matarajio mapana ya uwazi wa taarifa zinazoshikiliwa na taasisi za umma, na za binafsi zinazofanya kazi za uma au zinazofadhiliwa na fedha za umma;

(ii) Wajibu wa kuchapisha taarifa kwa upana zaidi na bila kushurutishwa/kuombwa;

(iii) Taratibu imara za kuandaa na kushughulikia maombi ambazo ni rahisi, bure na haraka (zikionyesha wazi muda wa kupata majibu/taarifa).

(iv) Orodha fupi ya taarifa zilizoruhusiwa zinazotokana na masuala ya ulinzi na usalama, maslahi ya umma yanaposhika hatamu na kukataliwa pale ambapo sehemu ya taarifa imeruhusiwa;

(v) Haki ya kukata rufaa.

(vi) Ulinzi kwa kutoa taarifa za nia njema na adhabu kwa kuzuia upatikanaji wa taarifa; na

(vii) Wajibu wa kutoa taarifa juu ya maombi yaliyopokelewa na kuhakikisha kuna adhabu zinatolewa kwa kukataa kutoa taarifa bila ya sababu za msingi.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Katiba na Sheria (MoCLA)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu (AG), AzaKi na sekta binafsi ambao hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: 1 Julai 2014 **Tarehe ya mwisho:** 31 Desemba 2014

AZIMIO KWA UJUMLA	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI			
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia na ubunifu kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Bado kuanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika
				✗	✗							✗		✗		

NI NINI KILIFANYIKA?

Azimio hili lina lengo la kutunga **sheria ya upatikanaji wa taarifa (ATI)** ambayo vuguvugu lake limeanzia azimio kama hili lililokuwamo lakini halikutekelezwa kwenye mpango kazi wa kwanza. Mpango kazi wa kwanza wa Tanzania wa OGP haukuwa na maelezo mahsusi ya undani wa sheria iliyokuwa ikitarajiwa; kwahiyo kupitia azimio hili serikali imezingatia mapendekezo ya taarifa ya tathmini ya IRM kwa mpango kazi wa kwanza wa OGP (2012–13). Mtafiti wa IRM alipendekeza wakati ule kuwa serikali ijumuishe azimio lililopitiwa upya, ikiwa ni pamoja na hatua zinazopimika, katika mpango wa pili (2014–16). Ilipendekezwa kuwa azimio lijumuishe michakato ya mashauriano kuelekea kuchapisha na kutunga sheria ya uhuru wa habari.

Azimio hili halikukamilika katika kipindi cha utekelezaji kinachofanyiwa tathmini kutokana na ukosefu wa mashauriano mapana na wadau, kulikosababisha mswada wa sheria ya ATI kutopitishwa bungeni mnamo mwaka 2015.

Kwa mwaka wote wa 2014 na mwanzoni mwa mwaka 2015, serikali ilianza mchakato wa kuandaa rasimu ya sheria ya ATI na ikafanya juhudi kuelekea utungwaji wake. Jaribio la kwanza lilikuwa kupitia mswada uliojulikana kama Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2013 mnamo Novemba 6, 2014, uliopendekezwa na Mwanasheria Mkuu aliyemaliza muda wake Frederick Werema. Bunge liliukataa muswada kwani ulikuwa na vifungu tata juu ya adahabu kali kuhusiana na uchapishaji wa habari za uchochezi. Kukataliwa kwa mswada huo kulipelekea pia kusitishwa kwa mchakato wa sheria ya ATI.[1]

Mnamo Juni 2015, serikali ikafanya jaribio la pili la kupitisha sheria ya ATI. Muswada ulipelekwa bungeni kwa hati ya dharura na hakukuwa na mashauriano ya kutosha na wadau. Muswada huo ulikataliwa bungeni na, kwa mujibu wa wadau wa jamii ya kiraia waliohojiwa, mchakato huo umesimama kwa sababu ya uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 25 Oktoba 2015.[2]

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanywa na mtafiti wa IRM, wadau wa jamii ya kiraia walieleza kuwa mchakato wa uandaaji rasimu ya miswada ya ATI, Vyombo vya Habari, na mingine miwili[3] ilikuwa na uharaka mno na ukosefu wa mashauriano na wadau, iliyopelekea jamii na baadhi ya wanaharakati wa haki za binadamu kukosoa mchakato na vilivyomo kwenye miswada kuwa haukuwa shirikishi au sikivu.[4] Baraza la Habari Tanzania (MCT), kati ya wengine, lilikuwa ni mojawapo ya waliochukua hatua ya kuhamasisha jamii juu ya masuala muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na mswada unaopendekezwa kupitia matangazo kwenye televisheni.[5]

NI NINI UMUHIMU WA AZIMIO HILI?

Azimio hili lilikuwa na athari ya mabadiliko makubwa. Kama lingetekelezwa, mswada na hivyo sheria inayofuata ingesaidia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa taarifa zinazoshikiliwa na serikali ambazo ni muhimu kwa watendaji wa jamii ya kiraia, sekta binafsi na hasa wananchi. Mtafiti wa IRM na wadau[6] wanaiona hii kama fursa iliyopotea kwa nchi kuonesha dhamira yake kwa tunu za OGP kwa kushughulikia changamoto kuu za kukuza uwazi na uadilifu kwa umma ndani ya serikali.

Ingawa wahojiwa kadhaa waliamini kuwa muswada wa ATI ulikuwa na vipengele chanya, ikiwa ni pamoja na wigo mpana na uwepo wa chombo cha usimamizi,[7] wengi walionelea kuwa mswada huo ulikosa kipengele kimoja muhimu: ulikosa wigo unaohitajika kisheria wa kufuta sheria tata na zilizopitwa na wakati, kama vile Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na Sheria ya Huduma za Utangazaji ya mwaka 1993.[8] Sheria hizo ambazo hazijafutwa zinazozungumziwa hapa, kwa mfano, zinaweza kusababisha gazeti, radio, au leseni ya kituo cha televisheni kusimamishwa au hata kufutwa kabisa na waziri mwenye dhamana bila ya kupewa nafasi au kuwapo mchakato wa haki ya kujitetea kisheria.

Baadhi ya wadau walikumbusha ukweli kuwa hakukuwa na nakala kwa lugha ya Kiswahili ya mswada kama inavyobidi, kitu ambacho kinadumaza fursa ya kutafakari mapendekezo yaliyokuwa yakitarajiwa kutoka kwa wananchi.

MUENDELEZO

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuwa serikali iboreshe juhudi zake kwa kushirikisha wadau wote muhimu kama hatua ya awali ya kufikia lengo kuu la kuwa na sheria ya ATI.

Wakati wa mkutano na wadau wa jamii ya kiraia uliofanywa na mtafiti wa IRM,[9] washiriki walipendekeza kuwa ndani ya miezi saba ijayo, maafisa wa serikali wafikirie yafuatayo:

- Miswada yote, ikiwa ni pamoja na ule wa rasimu ya ATI, utafsiriwe kwa Kiswahili na kusambazwa kwa wadau husika, kwa kutumia njia ya kufikisha nakala kwa mkono au kuweka mtandaoni.
- Mashauriano na wadau wakuu yafanyike kwa kutumia majukwaa mbalimbali ikiwemo mikutano ya ana kwa ana, vipindi vya moja kwa moja kwenye televisheni na redio, ujumbe mfupi wa maneno kwenye simu, na kushirikisha umma kupitia mitandao ya kijamii. Hii iwe ni sharti la uthibitishaji wa miswada yote ya sasa na baadae.
- Mfumo uwekwe ili kuingiza maoni yanayotokana na mashauriano na rasimu ya mswada kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi, kwa kuhakikisha kuwa muhtasari wa chapisho sahihi la rasimu ya mswada kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili zinawekwa kwenye tovuti ya wizara husika.
- Serikali ichukue rasimu ya mwisho na kuipeleka bungeni kwa majadiliano na hatimaye kupitishwa kuwa sheria ya ATI.

Mtafiti wa IRM anakubaliana na mapendekezo hayo ya wadau na anatanabahisha kuwa hatua kama zilizopendekezwa na wadau ni lazima zijumuishwe, zikiwa na tarehe zilizo wazi za kuanza na kumaliza, katika mpango kazi ujao wa OGP, ili utekelezaji wa azimio hili ukamilike ndani ya kipindi cha mpango kazi uliopo sasa (2014–16).

[1] Tanzania's Parliament Rejects Media Censorship Bill November 21, 2013 http://bit.ly/1VlUcG9, accessed 20 September 2015
[2] Anonymous. Telephone interview. 13 October 2015
[3] Miswada ya Makosa ya Kimtandao na Takwimu; hii miwili hatimaye ilipitishwa na bunge la Tanzania kwa hati ya dharura
[4] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[5] IRM researcher. Observation on local television. August-September 2014
[6] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[7] Centre for Law and Democracy. Tanzania: Note on the Draft Access to Information Act, 2015 May 2015 http://bit.ly/1o3X0Tw, accessed 22 September 2015
[8] Anonymous. Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[9] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015

3.2 | TAKWIMU HURIA

Maelezo kamili ya azimio:

Kuwa na mfumo wa takwimu huria hadi itakapofika Desemba 2016.

Hatua muhimu za utekelezaji wa azimio hili ni pamoja na zifuatazo:

(i) Kuanzisha chombo cha usimamizi au kikundi kazi chini ya Wizara ya Fedha ili kulitazama suala hili.

(ii) Miongozo itolewe, ikifuatiwa na maazimio ya kisheria yanayohimiza uwazi katika shughuli hizo na kuingiza dhana ya takwimu huria katika tafakuri za kisera, ikiwa ni pamoja na utoaji wa takwimu zinazoweza kusomwa na kompyuta/mashine nyingine.

(iii) Uanzishwaji wa tovuti kuu ya takwimu ambayo ni rahisi kuitumia, na shirikishi yaani data.go.tz.

(iv) Uchapishaji wa seti muhimu za takwimu katika data.go.tz, hususan sekta za elimu, afya na maji, ikiw ni pamoja na takwimu za Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) na mitihani ya taifa (NECTA), vituo vya madawa na Bohari Kuu ya Madawa (MSD), vituo vya maji, usajili wa kampuni, takwimu kuhusu sensa na utafiti na takwimu za kitaalamu zinazoonesha mipaka ya vijiji na kata; na kwa takwimu zote msisitizo uwekwe kwenye kutenganisha takwimu hadi kufikia ngazi ya vituo ili ziwe na manufaa kwa wananchi.

Shughuli za ziada kama zilivyoorodheshwa kwenye mpango wa utekelezaji:

- *Kupitia upya sera, sheria na kanuni za utoaji wa takwimu/data.*
- *Kutunga sera ya takwimu huria.*

Maoni ya uhariri: Hatua zilizohakikiwa katika azimio hili ni mchanganyiko wa hatua muhimu zilizomo ndani ya azimio lenyewe na shughuli zilizoelezwa katika mpango wa utekelezaji.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Fedha (MoF), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (POPSM), Wakala wa Mitandao ya Serikali (eGA), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (MoEVT), Wizara ya Maji (MoW), Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (MoHSW) na Ofisi ya Makumbusho ya Taifa.

Taasisi saidizi: Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PMO-RALG au OWM-TAMISEMI), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: Haikutajwa

Tarehe ya mwisho: 30 Juni 2016

AZIMIO KWA UJUMLA	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI			
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia na ubunifu kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Bado kuanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika
3.2. KWA UJUMLA			✗		✗			✗			✗			✗		
3.2.1.Chombo cha usimamizi			✗		✗					✗			✗			
3.2.2. Menejimenti ya takwimu			✗		✗						✗			✗		
3.2.3. Kupitia upya sera ya utoaji takwimu		✗			✗					✗			✗			
3.2.4. Sera ya takwimu huria		✗			✗						✗		✗			
3.2.5. Tovuti kuu ya takwimu huria			✗		✗			✗			✗					✗
3.2.6. Seti muhimu za takwimu kwenye tovuti kuu				✗	✗						✗				✗	

NI NINI KILIFANYIKA?

Azimio hili lina dira ya kuandaa mkakati wa takwimu huria ambao unajumuisha uundaji wa kanuni na sera, uundaji wa chombo cha usimamizi, na kuruhusu kuchapishwa kwa takwimu haraka iwezekanavyo katika tovuti kuu ya takwimu huria.

Kwa ujumla, azimio hili limeonesha utekelezwaji kwa kiasi kidogo. Hatua moja tu (3.2.5) ndio imetekelezwa kikamilifu na nyingine (3.2.6) inaonesha kutekelezwa kwa kiasi kikubwa. Hatua nyingine nne za mwanzo aidha hazijaanza kutekelezwa au zimetekelezwa kwa kiasi kidogo.

Kuhusiana na hatua ya kwanza (3.2.1), hakuna kikundi kazi wala chombo cha uratibu chini ya Wizara ya Fedha (MoF) kilichoundwa kusimamia utekelezaji wa azimio hili. Miongozo ya menejimenti ya takwimu huria (hatua ya 3.2.2), ilipaswa kuwa tayari hadi kufikia mwezi Oktoba 2014; hata hivyo, hadi tunapoandika taarifa hii, hakuna dalili ya mchakato wowote unaoendelea. Tathmini kama hiyo inaweza kusemwa kwa hatua 3.2.3 na 3.2.4 zinazohusu upitiaji upya wa sera ya takwimu na uandaaji wa sera ya takwimu huria.

Pamoja na hayo, wawakilishi wa jamii ya kiraia waliohojiwa na mtafiti wa IRM[1] walionelea kuwa hatua ya azimio 3.2.5—kama ilivyoandikwa kwenye mpango kazi—imetekelezwa kikamilifu baada ya kuanzishwa kwa tovuti kuu ya takwimu huria. Hatua 3.2.6

imekamilika kwa kiasi kikubwa baada ya seti za takwimu huria kadhaa kuchapishwa katika tovuti kuu hiyo. Mahojiano hayo yaliakisi ukweli kuwa serikali ilitambua na kutekeleza mapendekezo kutoka kwenye mpango wa kwanza kwa kuja na hatua 3.2.5, uanzishwaji wa tovuti kuu ya takwimu huria (www.opendata.go.tz), na 3.2.6, kuingiza mafungu ya takwimu huria kwa kiasi kikubwa.[2]

Kutokana na mahojiano,[3] mtafiti wa IRM aliarifiwa kuwa seti muhimu za takwimu zilizochapishwa kwenye tovuti kuu ya takwimu huria pia zitapatikana kwenye tovuti za wizara husika. Hadi sasa, ushahidi unaonesha kuwa ni wizara za Fedha na Maji tu zilizoweza kufanya hivyo, huku wizara ya Maji ikiwa na tovuti pekee kwa ajili ya utambuzi wa vituo vya maji.[4]

NI NINI UMUHIMU WA AZIMIO HILI?

Mkakati mpya wa takwimu huria ni hatua moja muhimu kuelekea upatikanaji wa taarifa kwa wananchi. Azimio lilikuwa na utashi mkubwa na liliandikwa vyema, likiwa na hatua zilizo wazi kueleweka na muda maalum wa kutekeleza kila hatua.[5]

Wadau wa AzaKi waliohojiwa na mtafiti wa IRM[6] waliisifu serikali kwa juhudi zake za kuboresha upatikanaji wa taarifa za serikali mtandaoni, kwani hapo awali ni watumishi serikalini na wafadhili tu ndio waliokuwa wakiruhusiwa kuzipata takwimu hizi. Wadau hao[7] walikuwa na maoni kuwa ilikuwa ngumu kuzitafuta takwimu hizo. Hata hivyo, mtafiti wa IRM aligundua kuwa, kinyume na madai ya wadau hao, takwimu hizo zilikuwa zikitafutika kirahisi na kuwa mfumo uliotumika katika kuzichapisha kwenye tovuti kuu ni ule uitwao comma-separated-values (CSV), unaoruhusu mafaili ya takwimu kutumika tena na watumiaji.[8]

Ni muhimu kujua kuwa serikali, kupitia mpango kazi uliopita, iliweza kuchapisha seti fulani za takwimu mtandaoni na katika mfumo unaosomeka na kompyuta/mashine. Hii ilikuwa ni pamoja na seti za takwimu kuhusu utambuzi wa vituo vya maji.[9] Pamoja na hayo, juhudi nyingi za serikali zilizokuwa zikitumia teknolojia zilitoa takwimu kwa mfumo ambao hausomeki kwa mashine/kompyuta kwa mfano PDF, JPEG na kadhalika.

Kwa mujibu wa mpango kazi wa sasa, tovuti kuu ya takwimu huria ilitakiwa kuwekwa seti za data/takwimu kutoka katika sekta tatu: elimu, afya na maji. Pia kuna wachangiaji wengine wengi wa data/takwimu mbali ya hizo wizara tatu, ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Bohari Kuu ya Madawa (MSD). Mtafiti wa IRM anathibitisha kuwa takwimu hizo zinapatikana katika tovuti kuu hiyo ingawa haziwekwi kwa muda muafaka, na zinapatikana kwa lugha ya Kiingereza pekee, lugha ambayo wananchi wengi hawaielewi. Kiswahili ni lugha ya taifa ambayo inazungumzwa na kiasi cha asilimia 99 ya watu wote waishio nchini Tanzania. Ili kuhakikisha kunakuwa na ushiriki na mrejesho wa watu kuhusiana na takwimu zinazochapishwa, ni muhimu kwa takwimu hizo pia zipatikane kwa lugha ya taifa-hata kama ni kwa lengo la kuwaelewesha wananchi.

Wadau wa AzaKi waliohojiwa[10] walitanabahisha kuwa hakuna ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa kuunda sera ya takwimu huria.[11]

MUENDELEZO

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuwa serikali ifanye juhudi za kumalizia utekelezaji wa hatua ambazo hajikamilika mpaka sasa hadi kufikia Juni 30, 2016. Kwa namna pekee, serikali izingatie kuandaa miongozo, kupitia na kuunda sera ya upatikanaji wa takwimu huria, ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uchapishwaji wa seti za takwimu/data siku zijazo.

Mtafiti wa IRM anakumbushia pendekezo kama hili lililofanywa wakati wa kutathmini utekelezaji wa mpango kazi wa kwanza wa OGP kuwa serikali iwe na wakala na kujengea uwezo ili uratibu wa takwimu uwe rahisi. Serikali pia, ihakikishe kunakuwa na taswira za takwimu zilizochapishwa kwenye tovuti kuu ya opendata.go.tz kwenye kila tovuti ya wizara husika, idara na / au wakala wengine wa serikali.

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuwa takwimu zipatikane kwa mfumo unawezesha kompyuta/mashine kuzisoma na zipatikane kwa lugha ya Kiswahili, ili ziweze kutafutwa na kutumika na wananchi.

IRM inapendekeza kuwapo kwa toleo la Kiswahili ama hata muhtasari wa takwimu unaochapishwa kwenye tovuti kuu; itasaidia watumiaji na michakato mingine yenye maslahi ya watu kuifanya tovuti tajwa na takwimu kuwa rafiki na kutumika zaidi.

Pia, uundaji wa sera za takwimu huria utakuwa na faida endapo majukwaa/mifumo ya wataalamu wa takwimu na mrejesho yatakuwa ni sehemu ya wadau.

[1] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[2] The open data portal http://opendata.go.tz/dataset when accessed on 21 October 2015 the portal had a total of 81 datasets disaggregated by organizations and data type/groups
[3] Anonymous. Face to face interview with IRM researcher. 5 October 2015
[4] Water point mapping http://bit.ly/1PUJKwZ accessed on 21 October 2015
[5] Start dates indiscernible as language used is time-frame
[6] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[7] ibid.
[8] The Open Data Institute, http://bit.ly/1PSbMmAaccessed on 31 December 2015
[9] Ngunga Tepani. Tanzania OGP IRM Report. March 2014
[10] Anonymous. Face to face interview with IRM researcher. 16 October 2015
[11] NYONYI: Tanzania yet to fully embrace openness, 25 October 2014, The Citizen, http://bit.ly/1KqdQGn accessed 31 December 2015

3.3 | UWAZI KATIKA BAJETI

Maelezo kamili ya azimio:

Kuwezesha upatikanaji wa takwimu za bajeti (taarifa muhimu nane) kwa umma , taarifa za ukaguzi za kamati za bunge na misamaha ya kodi hadi itakapofika Desemba 2014.

Kulingana na mifano bora ya kimataifa ya uwazi katika bajeti, hii itajumuisha:

(i) Kuchapisha, kwa wakati muafaka, taarifa muhimu za bajeti zifuatazo: taarifa kabla ya bajeti; muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; bajeti iliyopitishwa; bajeti ya wananchi; taarifa za kila mwaka juu ya mapato yaliyokusanywa, matumizi na madeni; mapitio ya nusu-mwaka; taarifa ya mwisho wa mwaka; na taarifa za wakaguzi.

(ii) Kuchapisha taarifa za Kamati za Ukaguzi za Bunge.

(iii) Kuchapisha misamaha ya kodi, kila mwezi.

(iv) Kuchapisha takwimu kuhusu bajeti mtandaoni, katika mfumo unaowezesha kusomwa na kompyuta/mashine pia taarifa muhimu zipatikane katika halmashauri za wilaya na katika ngazi ya chini kabisa kama vile vituo vinavyotoa huduma ya elimu na afya.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Fedha (MoF), Bunge, na ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PMO-RALG au OWM-TAMISEMI), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: 1 Julai 2014 **Tarehe ya mwisho:** 30 Juni 2016

AZIMIO KWA UJUMLA	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI			
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia na ubunifu kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Bado kuanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika
3.3. KWA UJUMLA				✗	✗		✗	✗			✗			✗		
3.3.1. Taarifa za bajeti za mwaka				✗	✗		✗				✗			✗		
3.3.2. Taarifa za kamati za ukaguzi za bunge				✗	✗		✗				✗		✗			
3.3.3. Misamaha ya kodi ya kila mwezi				✗	✗		✗					✗	✗			
3.3.4. Takwimu za bajeti zinazosomeka kwa mashine / kompyuta				✗	✗		✗	✗				✗	✗			

NI NINI KILIFANYIKA?

Azimio hili linaweka bayana lengo lenye utashi mkubwa la kuchapisha taarifa nane zifuatazo za bajeti kwa vigezo vinavyokusudiwa kuweka uwazi katika bajeti ili kufikia viwango vya kimataifa kwa mfumo ambao unawezesha takwimu kusomwa na kompyuta/mashine nyingine; taarifa kabla ya bajeti ; muhtsari wa mapendekezo ya bajeti; bajeti iliyopitishwa; bajeti ya wananchi; taarifa za kila mwaka juu ya mapato yaliyokusanywa, matumizi na madeni; mapitio ya nusu-mwaka; taarifa ya mwisho wa mwaka; na taarifa za wakaguzi.

Pamoja na uchapishaji mtandaoni, serikali iliazimia kuwa, taarifa za bajeti zipatikane kwa umma nje ya mtandao katika ngazi ya wilaya ikiwa ni pamoja na vituo vinavyotoa huduma ya elimu na afya. Kwa mujibu wa Kielelezo cha Uwazi katika Bajeti (OBI 2015), Tanzania ilipata alama zile zile za mwaka 2012, yaani 46 kati ya 100-inayochukuliwa kuwa dhaifu kwa uwazi katika bajeti. Pamoja na kuwa kuna maboresho katika utoaji wa taarifa za bajeti, taarifa muhimu mbili kati ya nane hazikuchapishwa, ambazo ni taarifa ya mapitio ya nusu-mwaka na ya mwisho wa mwaka. Kielelezo cha OBI 2015 pia kinaeleza kuwa mengi yangetekelezwa katika kuboresha ushiriki wa wananchi katika mchakato wa uandaaji bajeti.[1]

Mtafiti wa IRM kwa ujumla anaona kuwa azimio hili limetekelezwa kwa kiasi kidogo, kukiwa na takwimu zilizochapishwa chini ya hatua ya kwanza (3.3.1), ingawa si kwa wakati au kwa mfumo unaowezesha takwimu kusomwa na kompyuta/mashine nyingine. Kwa mfano bajeti ya wananchi kwa mwaka wa fedha 2014–15 ilipaswa kuchapishwa mtandaoni mnamo mwezi Aprili 2014 lakini haikuwa hivyo hadi mwezi Oktoba 2014, ilipopatikana kwenye tovuti ya asasi ya *Policy Forum*. Hii inadumaza umuhimu wa kuchapisha taarifa hiyo, ambayo ingeweza kutumiwa na wananchi mapema mwaka huo.[2]

Kiasi kidogo sana cha takwimu za bajeti, kinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha (MoF).

Taarifa za Kamati za Ukaguzi za Bunge (3.3.2) hazikupatikana kwenye tovuti za MoF, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) au Bunge.[3] Uchapishaji wa taarifa za misamaha ya kodi kila mwezi (3.3.3) na utoaji wa taarifa za bajeti katika mfumo unaowezesha kusomwa na kompyuta/mashine nyingine (3.3.4) bado haujaanza.[4]

NI NINI UMUHIMU WA AZIMIO HILI?

Azimio lina utashi na athari za wastani. Mtafiti wa IRM anaamini kuwa watendaji wa jamii ya kiraia na wengine walio nje ya serikali wangenufaika na taarifa ambazo zingechapishwa ili kufuatilia bajeti na kwa madhumuni ya ushawishi. Wadau wa AzaKi[5] wanaamini kuwa azimio hili, kama lingetekelezwa kikamilifu, lingewezesha kupatikana takwimu za bajeti na taarifa nyingine muhimu kwa kiasi kikubwa ambazo zilidhamiriwa kuwekwa mtandaoni. Wadau hao pia walitanabaisha kuwa pamoja na kuwa kiasi cha takwimu za bajeti zinazochapishwa na serikali ni muhimu, mchakato wa kushirikisha wananchi kupitia takwimu hizo ni muhimu pia kwa mrejesho. Taarifa ambazo hadi tathmini hii inaandikwa, zinapatikana japo kwa kiasi kidogo na pia hazikupatikana kwa muda muafaka, zinachukuliwa kuwa ni msingi mzuri wa mfumo rasmi wa uchapishaji takwimu za bajeti kwa siku za zijazo.[6]

Kupitia mahijiano, ilifahamika kuwa taarifa za bajeti zilikuwa zikikusanywa na kitengo mahsusi ndani ya taasisi kiongozi.[7] Hata hivyo, takwimu hizo hazichapishwi/hazitolewi mara kwa mara, kwani wizara zinazochangia zinapeleka takwimu zao katika muda wanaotaka wao.

MUENDELEZO

Mtafiti wa IRM anapendekeza yafuatayo:

- Wakala husika zimalize utekelezaji wa hatua ambazo bado hazijafikiwa.
- Jukumu la kuchapisha takwimu za bajeti na taarifa nyingine zinazohusiana, ziratibiwe na wakala/taasisi moja badala ya kutawanya kati ya taasisi kiongozi, wizara saidizi na vyombo vya umma.

Wadau sita wa jamii ya kiraia walipendekeza hatua zifuatazo zifikiwe kabla ya tarehe 30 Juni 2016:

- Kuimarisha wakala/kitengo cha uratibu ndani ya taasisi kiongozi iliyoteuliwa kukusanya, kuzifanyia kazi (ikibidi), na kuziingiza taarifa/takwimu kwenye tovuti kuu ya takwimu huria kwa wakati.

- Kuhakikisha kuwa seti za takwimu zote zinazowekwa mtandaoni zinapatikana katika mfumo unaowezesha kompyuta/mashine nyingine kusoma na zinawekwa kwa wakati.
- Kuwepo kwa mihutasari ya takwimu zote au nyingi zilizochapishwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuwa endapo hakutakuwa na hatua yoyote iliyofikiwa katika kipindi cha utekelezaji wa mpango kazi uliopo, basi azimio hili lijumuishwe katika mpango ujao wa OGP.

[1] Open Budget Index, 2015, http://bit.ly/1TDRNxY, accessed 20 September 2015
[2] Citizens Budget 2014-15http://bit.ly/1NQht3b accessed on 20 September 2015
[3] A search on http://www.parliament.go.tz/committee-reports-list drew a blank on parliamentary audit committee reports
[4] URT. Tanzania Open Government Partnership (OGP) Second National Action Plan 2014–15 and 2015–16. June 2014
[5] Stakeholders meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[6] ibid
[7] IRM researcher telephone interview with PMO-RALG official, 26 September 2015

3.4 | UWAZI KATIKA MASUALA YA ARDHI

Maelezo kamili ya azimio:

Kuhakikisha kuwa kuna upatikanaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, umiliki na maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa mtandaoni kwa matumizi ya umma hadi itakapofika Juni 2016.

Hii inajumuisha mambo yafuatayo:

(i) Kuchapisha taarifa za maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo (ukulima na ufugaji)

(ii) Kuchapisha mipango yote ya matumizi ya ardhi na kufanya yawafikie wananchi kuanzia ngazi ya taifa hadi ya msingi.

(iii) Kuweka mtandaoni kanzi ya takwimu za umiliki ardhi ambazo ni rahisi kuzitafuta.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHHSD)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (PMO-RALG au OWM-TAMISEMI), Kituo cha Uwekezaji (TIC), AzaKi na asasi za sekta binafsi ambazo hazikutajwa

Tarehe ya kuanza: Haikutajwa **Tarehe ya mwisho:** 31 Desemba 2015

AZIMIO KWA UJUMLA	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI			
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia na ubunifu kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Bado kuanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika
3.4. KWA UJUMLA			✗		✗			✗			✗			✗		
3.4.1. Maeneo yaliotengwa			✗		✗						✗			✗		
3.4.2. Mpango wa matumizi ya ardhi			✗		✗						✗			✗		
3.4.3. Kanzi ya takwimu za umiliki ardhi mtandaoni			✗		✗			✗				✗	✗			

NI NINI KILIFANYIKA?

Azimio hili lina dhamira ya kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa haki na usawa wa masuala ya ardhi kwa kupitia uchapishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, taarifa za umiliki, na maeneo yaliyotengwa. Serkali iliazimia kuchapisha, pamoja na mambo mengine, maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo (kwa mfano, ukulima na ufugaji) na kuweka mtandaoni kanzi ya takwimu za umiliki wa ardhi nchini Tanzania ambazo ni rahisi kuzitafuta.

Azimio hili limetekelezwa kwa kiasi kidogo. Wadau wa jamii ya kiraia wanakubaliana na tathmini hii ya IRM, wakionesha masikitiko yao kwa serikali kushindwa kutekeleza azimio hili, kwani baadhi ya takwimu hizi zingeweza kupatikana kirahisi kama ambavyo ilivyoelezwa kwenye taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi.[1]

Wakati wa mahojiano kati ya IRM na mmoja wa maafisa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (MLHHSD), afisa huyo alieleza kuwa fedha kutoka mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) umeiwezesha serikali kupima viwanja na mashamba katika wilaya nne za mkoa wa Morogoro. Taarifa hii haipo kwenye tovuti ya wizara wala mahali popote ambapo afisa huyo wa wizara / MLHHSD alitaja ukosefu wa maafisa wenye ujuzi wa kuchakata taarifa zilizokusanywa na kuziweka mtandaoni.[2]

Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Ardhi / MLHHSD, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs), na wadau wengine wameweka lengo la kutoa Vyeti vya Umiliki wa Ardhi Kimila (CCROs) kiasi cha milioni kumi ndani ya miaka mitatu. Chini ya programu ya Mpango wa Kusaidia Umiliki wa Ardhi (LTSP), angalau vyeti / CCRO milioni sita vinaweza kutolewa. Lengo la programu hii, pamoja na mambo mengine, ni kuhakikisha kuwa kuna utoaji wa haki ya umiliki wa ardhi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za umiliki wa ardhi kwa ajili ya matumizi ya biashara ambayo yanaweza kutengwa kwa uwekezaji.[3] Wabia wengine ambao wamechangia katika ajenda ya kitaifa ya maboresho ya ardhi ni pamoja na mfuko wa IFAD kupitia Wizara ya Kilimo, na Benki ya Dunia, ambayo inaifadhili serikali katika kuunda mfumo wa taarifa za usimamizi wa rasilimali ardhi nchini. (ILMIS), ambao bado upo katika hatua za majaribio. Mfumo wa ILMIS utakuwa ni rasilimali ya kielektroniki kitaifa ambayo imeundwa ili kuboresha rejesta ya ardhi nchini, ambayo itapatikana na kuwiana na taarifa zilizopo katika ngazi za wilaya na manispaa.

Wadau wa jamii ya kiraia walikuwa na ufahamu wa juhudi zilizokuwa zikifanywa ili kutekeleza hatua ya tatu (3.4.3) ya azimio hili, lakini wengi hawakuwa na taarifa kuhusu utekelezaji wa hatua nyingine mbili za mwanzo (yaani 3.4.1 na 3.4.2) za azimio hili.[4]

NI NINI UMUHIMU WA AZIMIO HILI?

Azimio hili linaweka hatua muhimu sana kuelekea kufanya usimamizi wa ardhi kwa uwazi zaidi. Watafiti kadhaa wametambua ukosefu wa mipango ya matumizi ya ardhi, kinachodhaniwa kuwa ni wimbi la "uporaji ardhi"," ongezeko la uwekezaji mkubwa katika kilimo, sera na taasisi dhaifu, viongozi wasio waadilifu na kutowaamini wafugaji kama sababu zinazochangia migogoro ya mara kwa mara.[5] Nchini Tanzania, ardhi inamilikiwa na serikali kuu, ambavyo vinasimamia katika ngazi za wilaya au manispaa na kijiji ama mtaa.

Watu binafsi hawamiliki ardhi bila kikomo. Hii ni kutokana na kuwa hati ya kumiliki ardhi inaweza kutolewa kwa miaka 33 kwa wawekezaji au miaka 99 kwa raia wa Tanzania, kama watapenda kumiliki ardhi iliyopimwa. Pamoja na juhudi za hivi karibuni za serikali za kutaka hati za umiliki ardhi kimila / CCRO milioni kumi zitolewe kwa vijiji, kumekuwa na migogoro kadhaa ya ardhi nchi nzima ambayo haijapatiwa ufumbuzi, hususan kati ya jamii za wafugaji na wakulima ambazo huishi jirani kwenye vijiji au kata. Wananchi pia wana ugomvi, na wawekezaji ambapo wakulima/wananchi mara nyingi huwatuhumu wawekezaji kuwa ni waporaji wa ardhi.[6]

Kwahiyo ni muhimu kwa serikali kuboresha upatikanaji wa taarifa na uwazi katika masuala yanayohusu matumizi ya ardhi. Hivyo basi, ni muhimu kwa serikali ikachapisha mipango ya matumizi ya ardhi, na kuweka wazi taarifa juu ya maeneo yaliyotengwa kwa uwekezaji mkubwa wa kilimo, na kuwa na kanzi ya takwimu za ardhi mtandaoni.

Wadau wa jamii ya kiraia wanaamini kuwa azimio hili ni hatua kubwa kuelekea katika usimamizi wa matumizi ya ardhi kwa haki na usawa nchini Tanzania.[7] Wanadai kuwa matumizi ya ardhi na usimamizi wake umekuwa ni kero ya muda mrefu nchini ikithibitishwa na migogoro isiyokwisha kati ya wakulima na wafugaji na kashfa

za rushwa zinazohusisha tuhuma dhidi ya vigogo serikalini. Uwazi katika masuala ya ardhi ungeweza kuweka usahihi wa taarifa za matumizi ya ardhi na wamiliki pale ambapo taarifa hizi hazijawahi kutolewa kwa umma. Kanzi ya takwimu za umilki ardhi (au ILMIS) inaweza kuisaidia serikali kushughulikia tatizo la wananchi kukosa uaminifu kwake katika kusimamia ardhi nchini, kwani itaweka wazi taarifa zote za umiliki wa ardhi hapa nchini.

Hata hivyo, azimio hili pekee halioneshi mabadiliko makubwa ya namna ardhi inavyosimamiwa nchini.

Endapo serikali ingekuwa na wafanyakazi wa kutosha katika kitengo cha Mifumo ya Usimamizi wa Taarifa (MIS) katika wizara ya ardhi / MLHHSD, azimio hili lingetekelezwa kwa kiasi kikubwa.

MUENDELEZO

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuwa serikali imalizie utekelezaji wa azimio hili bila kukawia. Wahojiwa kutoka AzaKi pia wanaamini kuwa yafuatayo yafanyike ili kukamilisha utekelezaji wa azimio hili:[8]

- Kuimarisha idara ya TEHAMA au MIS katika wizara ya ardhi / MLHHSD ili iweze kuchapisha takwimu zinazohusiana na azimio hili.
- Kuweka mtandaoni takwimu na taarifa nyingine zinazohusiana na ardhi mtandaoni, ikiwa ni pamoja kanzi katika mfumo unaowezesha takwimu kusomwa na kompyuta/mashine nyingine.
- Taarifa zichapishwe kwa lugha zote, yaani Kiswahili na Kiingereza hadi kufikia Juni 30, 2016.

Mwakilishi wa mtandao wa AzaKi zinazoshughulika na masuala ya ardhi hapa nchini – (HAKIARDHI), alipendekeza azimio hili liwekwe tena katika mpango kazi ujao wa OGP hapa nchini huku akiitaka serikali kuwahusisha wadau wengi zaidi katika utekelezaji wake.[9]

Wadau katika mkutano wa AzaKi walionelea kuwa azimio hili lisiwekwe peke yake bali liunganishwe na maazimio mengine yanayotaka upatikanaji wa takwimu huria kwenye mpango kazi ujao wa OGP wa Tanzania, kama vile maazimio kuhusu takwimu za kisekta, bajeti na tasnia ya uziduaji.[10] Hata hivyo, mtafiti wa IRM ana maoni kuwa kuunganisha maazimio au kuwa na hatua nyingi kwenye azimio moja kunaweza kuathiri utekelezaji na kupunguza hadhi / umuhimu wa uwazi katika usimamizi wa ardhi.

[1] Stakeholder meeting. Dar es Salaam, 25 September 2015
[2] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher 21October 2015
[3] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 02 January 2016
[4] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[5] Godfrey Massay, TNRF. A Coalition of Farmers and Pastoralists; An Alternative Paradigm to Resolving Land Use Conflicts. 15 January 2016. http://bit.ly/1Stwpwg, accessed 21 January 2016
[6] Songa wa Songa, Citizen Reporter. SPECIAL REPORT: Land grabbing in Tanzania: The truth, fallacies and fights. http://bit.ly/1NQuGc8, accessed 20 January 2016
[7] Ibid.
[8] Drawn from telephone interviews with stakeholders. 13 October 2015
[9] Anonymous. Face to face interview with the IRM researcher. 16 October 2015
[10] Ibid.

3.5 | UWAZI KATIKA TASNIA YA UZIDUAJI

Maelezo kamili ya azimio:

Tanzania itekeleze maazimio yake ya EITI hadi kufikia Juni, 2015

Hii inajumuisha mambo yafuatayo:

(i) Kuchapisha mikataba ya uendelezaji wa madini (MDAs) na Kandarasi za Kugawana Faida (PSCs) ya tangu 2014 na kuendelea itakapofika Juni, 2015;

(ii) Kunakili sera ya serikali kuhusu utoaji wa taarifa za kandarasi au mikataba iliyosainiwa kabla ya Juni, 2015; na

(iii) Kuchapisha maeneo yaliyotengwa kwa uchimbaji madini hadi kufikia Desemba, 2014.

Taasisi kiongozi: Wizara ya Nishati na Madini (MEM)

Taasisi saidizi: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Tarehe ya kuanza: Haikutajwa **Tarehe ya mwisho:** 31 Desemba 2015

AZIMIO KWA UJUMLA	UMAHSUSI				UHUSIANO NA TUNU ZA OGP				ATHARI TARAJALI				UTEKELEZAJI			
	Hakuna	Mdogo	Wastani	Uko juu	Upatikanaji taarifa	Ushiriki wa wananchi	Uwajibikaji kwa umma	Teknolojia na ubunifu kwa ajili ya uwazi na uwajibikaji	Hakuna	Ndogo	Wastani	Mabadiliko makubwa	Bado kuanza	Kiasi kidogo	Kiasi kikubwa	Umekamilika
3.5. OVERALL				✗	✗		✗				✗			✗		
3.5.1. Kuchapisha MDAs na PSCs tangu 2014 na kuendelea				✗	✗		✗					✗		✗		
3.5.2. Utoaji taarifa mikataba iliyosainiwa kabla ya 2014				✗	✗		✗				✗		✗			
3.5.3. Kuchapisha taarifa za maeneo yaliyotengwa kwa uchimbaji madini				✗	✗		✗				✗		✗			

NI NINI KILIFANYIKA?

Azimio hili lina dhamira ya kutekeleza wajibu wa Tanzania kama nchi mwanachama wa EITI hadi kufikia Juni 2015. Tanzania ilitangazwa rasmi kuwa ni nchi iliyokidhi masharti ya uanachama wa mpango wa kuhamasisha uwazi katika tasnia ya uziduaji (EITI)– mnamo tarehe 12 Desemba 2012. Hata hivyo, nchi ilisimamishwa uanachama kwa muda, mnamo Septemba 2015 ikiwa ni matokeo ya kushindwa kuchapisha taarifa ya mwaka 2012–13 kama tarehe ya mwisho iliyopangwa ambayo ni Juni 30, 2015.

Licha ya tovuti ya Wizara ya Nishati na Madini kuwa na taarifa za makampuni ya madini yaliyosajiliwa, yakiwa na maelezo ya kina ya umiliki, na hata baada ya bunge kupitisha sheria ya Uwazi katika EITI, azimio limehesabiwa kuwa halijaanza kutekelezwa. Hatua hizo muhimu zilizofikiwa na serikali, ingawa zina uhusiano wa karibu sana na azimio hili, hazikuwa sehemu ya hatua za azimio hili kama lilivyoandikwa.

Pamoja na kuwa ilikuwa nje ya muda wa tathmini hii, kusimamishwa uanachama wa EITI kuliondolewa mnamo Desemba 17, 2015 baada ya taarifa za mapato kwa kipindi cha 2012–13 na 2013–14 kuchapishwa mnamo tarehe 27 Novemba 2015.[1]

Hata hivyo, huku ikiwa imesimamishwa uanachama, serikali ya Tanzania ilifanya shughuli kadhaa kuhusiana na sera ya jumla ya tasnia ya uziduaji nchini. Mnamo Julai 2015, bunge lilipitisha miswada mitatu (kati ya mingine kadhaa), ambayo ililetwa na serikali kwa hati ya dharura, kuwa sheria. Sheria hizi ni Sheria ya uwazi na uwajibikaji katika tasnia ya uziduaji ya mwaka 2015 (EITAA), Sheria ya petroli ya mwaka 2015, na Sheria ya usimamizi wa mapato yatokanayo na gesi na mafuta ya mwaka 2015. Hadi kufikia Agosti 2015, sheria hizi tatu zilikuwa zimeshapitishwa na bunge na kusainiwa na Rais.[2]

Kati ya sheria hizo tatu, EITAA ndiyo sheria ambayo inahusika moja kwa moja na ina umuhimu katika utekelezaji wa azimio hili, kwavile inasisitiza kuweka wazi mikataba ya uzalishaji na kugawana faida. EITAA ni sheria muhimu kwa utekelezaji wa azimio hili na katika kuzuia hali iliyojitokeza kupelekea nchi ya Tanzania kusimamishwa uanacama wa EITI: yaani kucheleweshа uchapishaji wa taarifa za kifedha katika sekta ya uziduaji.

Sheria hizi zilihuisha na kuweka pamoja sheria zilizokuwepo kabla kwa sekta ya gesi na mafuta. Lengo lingine la sheria hizo lilikuwa ni kufuta sheria za awali mbili, ambazo ni Sheria ya Petroli (uchunguzi na uzalishaji) ya mwaka 1980, iliyokuwa ikihusu shughuli za petroli na ile ya Petroli ya mwaka 2008, iliyokuwa ikihusu shughuli za kati na chini za ugavi wa petroli.

Kwa mujibu wa mtendaji mmoja wa jamii ya kiraia aliyehojiwa,[3] kanuni za kufanya sheria zilizopitishwa kuanza kufanya kazi, ikiwa ni pamoja na mifumo muhimu, bado inaandaliwa. Kikundi cha wadau mbalimbali cha TEITI (TEITI-MSG) ni kamati ya uangalizi inayoundwa na wawakilishi kutoka serikalini na jamii ya kiraia nchini Tanzania ambacho kinasimamia uwajibikaji kwa EITI na kutoa ushauri katika michakato ya sera na sheria. Mtafiti wa IRM aliarifiwa kuwa TEITI-MSG imeanza kuandaa kanuni za sheria ya EITAA ya mwaka 2015 ambazo baadae zitapelekwa kwenye baraza la mawaziri kwa ajili ya kupitishwa.

Sheria ya EITAA itasaidia hatua 3.5.1 ya azimio hili kutekelezwa kwa ukamilifu katika siku zijazo. Kutokana na mashauriano yanayoendelea ya kuzifanya kanuni kuanza kutumika, kunamaanisha kuwa utekelezaji wa hatua 3.5.2 & 3.5.3 za azimio hili haujaanza.

NI NINI UMUHIMU WA AZIMIO HILI?

Azimio hili ni hatua ya kuelekea katika njia sahihi kulikofanywa na serikali ya Tanzania kuhakikisha kuwa usimamizi wa tasnia ya uziduaji unafanyika kwa ufanisi na uwazi, ambayo kwa sasa inachangia asilimia nane (8%) ya jumla ya pato la serikali.[4]

Wadau kutoka jamii ya kiraia wanadhani kuwa serikali ingeweza kuwa na utashi zaidi kuweka wazi mikataba au taarifa za EITI, hata ile iliyosainiwa kabla ya mwaka 2014. Kwa mfano, serikali ingeweza kuliandika upya azimio hili ili lichapishe taarifa za mikataba ya tasnia ya uziduaji iliyoingiwa na serikali kabla ya mwaka 2014, ikiwa ni tofauti kabisa na kilichomo kwenye mpango kazi uliopo sasa.[5] Huko nyuma, vyombo vya habari vimetaarifu kuhusu kashfa za rushwa zinazohusu mikataba katika sekta ya madini. Kwa mfano, wadau[6] wanaamini kuwa rushwa na kubebana zimechangia sana katika kusaini kwa kificho mikataba ya MDAs na PSAs za gesi kati ya serikali na makampuni yanayowekeza katika tasnia ya uziduaji kwa mikataba iliyosainiwa kabla ya mwaka 2014.

Mwanzoni mwa mwaka 2014, mkataba uliovujishwa kwenye vyombo vya habari nchini ulionyesha kuwa kampuni ya Exxon Mobil na Statoil (kutoka Norway) zingeilipa Tanzania mrabaha usiozidi asilimia hamsini (50%) ya faida kutoka katika kitalu cha gesi asilia kilichopo Bahari ya Hindi. Taarifa hizi zilisababisha zogo kutoka kwa wananchi, wabunge, na jamii ya kiraia, ambao waliitaka serikali kuweka wazi mikataba yote.[7] Kwa kawaida serikali huwa haiweki wazi taarifa kama hizi na huhodhi maelezo mengine ya kina ya mikataba ya mafuta, gesi na madini. Baadaye, watumishi waandamizi wa Shirika la maendeleo ya petroli (TPDC) walifikishwa mahakamani, kufunguliwa mashtaka ya kukiuka taratibu ya kuweka wazi PSA za mafuta na gesi. Maafisa hao waliokuwa wakituhumiwa walijitetea kuwa kutokuweka wazi huko kulitokana na vifungu vya usiri vilivyokuwemo kwenye mikataba hiyo.

Kamati ya bunge ya fedha za umma (PAC) iliitaka TPDC kuhakikisha kuwa inawapa mikataba yote 26 ya mafuta na gesi kabla ya tarehe 3 Novemba, 2014. Baadaye, mwenyekiti wa PAC Mh. Zitto Kabwe (Mbunge) na maafisa wa mwekezaji Statoil walithibitisha kuwa usiri ni suala la serikali kwani hakukuwa na vifungu vyovyote vya usiri katika mikataba hiyo ya PSA.[8]

Mtafiti wa IRM anaamini Tanzania ina uwezo wa kusimamia rasilimali zake kwa njia za uwazi na uwajibikaji zaidi na kuepuka kile kinachojulikana kama laana ya rasilimali iliyozikumba nchi kadhaa ambao zina utajiri wa rasilimali.[9] Wadau wa jamii ya kiraia[10] waliisifu serikali ya Tanzania kwa kuendelea kushiriki kama sehemu ya nchi tisa za EITI zinazoweka wazi umiliki wa makampuni ya tasnia ya uziduaji kuwa mfano bora wa kukuza uwazi.[11]

Hata hivyo, wadau[12] waliikosoa sheria iliyopitishwa hivi karibuni ya Petroli ya mwaka 2015, kwani ina kifungu kinachotaka mtafutaji taarifa zinazohusu mikataba kulipia ada kwa mikataba, leseni na vibali vya zamani hapa nchini—kitu ambacho ni kinyume na uwazi na upatinakaji wa taarifa unaodhamiriwa na EITI.

MUENDELEZO

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuwa yafuatayo yafanyike ili kukamilisha utekelezaji wa azimio:

- Kuchapisha mikataba yote ya MDA na PSC ya kuanzia mwaka 2014 na kuendelea, kwa njia za mtandaoni (kupitia tovuti kuu ya takwimu huria au tovuti ya wizara ya Nishati na Madini) na nje ya mtandao hadi kufikia Juni 30, 2016.
- Kuchapisha sera ya serikali ya kilichokuwa kikifuatwa wakati wa kutoa taarifa za mikataba iliyosainiwa kabla ya mwaka 2014, itakapofika Juni 30, 2016, kwa njia za ndani na nje ya mtandao.
- Serikali ichapishe takwimu za maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya utafutaji wa madini, mafuta na gesi kwa lugha zote za Kiswahili na Kiingereza , kwa mfumo unaowezesha takwimu hizo kusomwa na kompyuta/ mashine zingine itakapofika Juni 30, 2016.

[1] Tanzania: More revenues from extractives despite falling prices, 17th December, 2015, http://bit.ly/1PVdrhB, accessed 15 January 2016
[2] Tanzania's New Regime on Oil and Gas Laws; Unveiling Knights or Villains? August 10, 2015 http://bit.ly/1P7BkyU accessed on 21 October 2015
[3] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 02 January 2016
[4] The importance of natural resources for government revenues. EITI. http://bit.ly/1SYFfSc accessed on 20 October 2015.
[5] Anonymous. Telephone interview with IRM researcher. 6 September 2014
[6] Stakeholder meeting. Dar es Salaam. 25 September 2015
[7] Kizito Makoye. Top Tanzania officials arrested in row over oil, gas contracts. November 4, 2014 http://tmsnrt.rs/1nHxovp accessed on 20 October 2015.
[8] Ben Taylor. Apparently-everyone-wants-transparency-in-tanzanias-gas-contracts-lets-get-them-online http://bit.ly/1Piu2X0 accessed on 20 October 2015.
[9] Referring here to natural resource extraction related corruption.
[10] Stakeholder meeting. Dar es Salaam, 25 September 2015
[11] Rasmus Hundsbæk Pedersen and Peter Bofin. The politics of gas contract negotiations in Tanzania: a review. http://bit.ly/1Piu6Wy accessed on 20 October 2015.
[12] Ben Taylor.Tanzania Extractive Industries Draft Laws Transparency http://bit.ly/1NQRXKV accessed on 20 October 2015.

V | MCHAKATO: KUJITATHMINI

Orodha ya kujitathmini

Taarifa ya mwaka ya utekelezaji ilichapishwa au kutolewa?	Hapana
Je, ilitoka kwa wakati uliopangwa?	Hapana
Taarifa hiyo inapatikana kwa lugha ya Kiswahili?	Hapana
Taarifa inapatikana kwa lugha ya Kiingereza?	Hapana
Je, serikali ilitoa notisi ya muda wa wiki mbili kwa wananchi/umma kutoa maoni yao kuhusu rasimu ya taarifa ya utekelezaji ambayo serikali ilijitathmini?	Hapana
Kuna maoni yoyote yaliyopokelewa kutoka kwa wananchi?	Hapana
Je, taarifa ya kujitathmini inapatikana kwenye tovuti kuu ya OGP?	Hapana
Je, taarifa ya tathmini ya utekelezaji ya serikali ilionesha mapitio ya juhudi za mashauriano wakati wa kuandaa mpango kazi?	Hapana
Je, taarifa ya kujitathmini ilionesha mapitio ya juhudi za mashauriano wakati wa utekelezaji wa mpango kazi?	Hapana
Je, taarifa ya kujitathmini ilitoa maelezo juu ya muda uliotengwa kwa wananchi kutoa maoni wakati wa kuandaa taarifa hiyo?	Hapana
Je, taarifa ilihusu maazimio yote?	Hapana
Je, taarifa ilitathmini kila azimio kwa kutazama muda na hatua zilizomo kwenye mpango kazi?	Hapana
Je, taarifa ilizingatia mapendekezo muhimu ya IRM (kwa 2015+ pekee)?	Hapana

MUHTASARI WA TAARIFA ZA ZIADA

Serikali ya Tanzania haikutoa taarifa ya mwaka ya kujitathmini hadi kufikia tarehe 30 Septemba 2015 ambayo ilikuwa ndiyo mwisho wa kupokea taarifa kwa mujibu wa OGP. Hakukuwa na maoni yaliyoandaliwa au kutolewa pale IRM ilipoomba.

Wadau wa jamii ya kiraia[1] walitanabahisha kuwa serikali haikuzitafuta AzaKi kwa ajili ya uandaaji taarifa hiyo ya kujitathmini na kuelezea masikitiko yao kuwa AzaKi hazikushirikishwa vya kutosha kwenye utekelezaji wa mipango kazi ya OGP yote miwili, yaani wa kwanza na wa pili.

UFUATILIAJI WA MAPENDEKEZO YA AWALI YA IRM (2015 NA KUENDELEA)

Wakati wa tathmini ya mpango kazi uliopita wa OGP (2012–13), mtafiti wa IRM alipendekeza serikali ijumuishe masuala kadhaa yanayomjali mtumiaji katika mpango kazi unaofuata:

1. Kuandaa maazimio huku nia ikiwa ni kuboresha uwezo wa wananchi kushirikiana na watendaji/ watumishi serikalini moja kwa moja.
2. Kutoa takwimu mtandaoni katika mfumo unaowezesha takwimu kusomwa na kompyuta/ mashine nyingine na hata mifumo tofauti na hiyo (yaani, PDF, JPEG na kadhalika), ili kuhakikisha kuwa taarifa zilizochapishwa zinafikiwa na watu wengi . Hii ni pamoja na takwimu kama vile BEST, mifumo ya ramani za vituo vya maji, na misamaha ya kodi iliyopitishwa ili wadau waweze kuzitumia na kuzichambua taarifa hizo. Taarifa zingine, kama vile mapato na matumizi au jambo lolote linalohusu kuwapa taarifa wananchi, zinaweza kuchapishwa katika mifumo isiyosomeka na kompyuta/mashine nyingine.
3. Kufanya taarifa zote au nyingi ya hizo na takwimu kadhaa zipatikane kwa umma kwa lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha rahisi kueleweka.

Ukiondoa maazimio mawili kwenye mpango kazi wa pili wa OGP (2014–16), mapendekezo hayo hayakuzingatiwa. Maazimio ambayo kwa kiasi fulani yamezingatia vigezo hapo juu ni yale ya kuwa na tovuti kuu ya takwimu huria na uchapishaji wa seti za takwimu za bajeti katika mfumo unaowezesha kompyuta/ mashine nyingine kuzisoma huku kukiwa na muingiliano kiasi kati ya taarifa na mtumiaji / mwananchi.

[1] Stakeholder meeting. Dar es Salaam, 25 September 2015

VI | MUKTADHA KITAIFA

Ni mapema mno kuamua endapo mafanikio ya juhudi za hivi karibuni za kushughulikia changamoto za rushwa iliyokithiri na kutowajibika kwa watumishi wa umma nchini Tanzania, kwa hapa zilipofikia, kuwa ni endelevu. Juhudi za ziada zinahitajika ili kuboresha uhuru wa kujieleza na kushughulikia rushwa iliyotamalaki katika ngazi za juu za utumishi wa umma. Kufuta usiri uliopo katika usimamizi wa rasilimali za nchi, ikiwa ni pamoja na tasnia ya uziduaji na umiliki ardhi, zitakuwa na jukumu kubwa la kuitoa serikali ilipo sasa kiutendaji katika kuelekea kuwa na serikali ambayo inatenda kwa uwazi na inawajibika kwa wananchi wake.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepiga hatua kubwa sana katika kupambana na rushwa katika muongo mmoja uliopita. Mnamo mwaka 2006, serikali ilipitisha Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa ambao ulionesha nia ya serikali ya kuingiza haki za msingi katika katiba yake, kama vile haki ya kupata taarifa, ulinzi kwa raia wema wanaotoa taarifa zinazosaidia kukamatwa kwa wahalifu na haki yao ya kutojulikana ni akina nani na uridhiaji wa makubaliano ya kimataifa na taasisi za haki za binadamu.[1]

Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCA) ndiyo sheria pekee kimsingi inayomtia mtu hatiani kwa masuala yanayohusiana na, pamoja na mengine, kujaribu kutoa rushwa, kughushi, kuhonga, na kutakatisha fedha. Hata hivyo, kwa mujibu wa shirika la *Transparency International*, Tanzania ina alama 31 kati ya 100 katika faharasa ya maoni ya rushwa ya mwaka 2015 (CPI) – ambacho hupimwa kwa alama sifuri (kuwa ndiyo rushwa imekithiri zaidi) hadi kufikia mia moja / 100 (safi kabisa / hakuna rushwa). Tanzania pia ni nchi ya 117 kati ya nchi 165 katika faharasa hiyo.[2] Kwa kupata alama ndogo hivyo inadhihirisha mtazamo kuwa rushwa bado ni tatizo na ipo kila mahali hapa Tanzania na kwa sekta mbalimbali za uchumi, ikiwa ni pamoja na manunuzi ya serikali, usimamizi wa ardhi, kodi, forodha[3] na tasnia ya uziduaji.[4]

Kwa mfano mapema mnamo mwaka 2014, aliyekuwa mtendaji mkuu wa shirika pekee la ugavi wa umeme nchini Tanzania (*Tanzania Electricity Supply Company* — TANESCO), alishitakiwa kwa matumizi mabaya ya madaraka na kugushi. Ukaguzi wa serikali ulimtuhumu wakati wa kutoa zabuni ya zaidi ya Shilingi za Kitanzania 884,000,000 (au Dola za Kimarekani 524,000) kwa kampuni ambayo ilikuwa ikimilikiwa kwa pamoja yeye na mkewe.[5] Baadaye mwaka huo huo, TANESCO iliikuwa ikimulikwa tena, ambapo uhamishaji wa angalau Dola za Kimarekani 120,000,000 kutoka akaunti ya Tegeta Escrow kwenda kampuni ya *Independent Power Tanzania Limited* (IPTL) ilikuwa ndiyo kashfa mpya kuitingisha serikali iliyokuwapo madarakani. Akaunti ya Tegeta Escrow ilianzishwa kwa pamoja kati ya TANESCO na IPTL kwa ajili ya kutunza fedha mnamo mwaka 2006 huko Benki Kuu (BoT) wakati ambapo wawili hao wakisubiri matokeo ya malumbano ya kesi kuhusiana na gharama za uzalishaji iliyokuwa ikirindima katika mahakama hapa nchini na nje ya nchi. IPTL ni kampuni tanzu iliyoundwa kwa pamoja kati ya *Mechmar Corporation* ya Malaysia (inayomiliki asilimia 70 ya hisa za IPTL) na VIPEM ya Tanzania (inayomiliki asilimia 30 ya hisa za IPTL).

Wafadhili wa kimataifa waliamua kusitisha misaada wakati sakata hilo likiendelea ambapo maazimio ya kutoa msaada na mikopo kwa Tanzania yalishuka kutoka asilimia 21 ya bajeti ya Tanzania kwa mwaka wa fedha 2013-14 hadi kufikia asilimia 15 kwa mwaka wa fedha 2014-15. Aliyekuwa Rais wakati huo, Jakaya Kikwete, aliwafukuza kazi mawaziri wawili ambao walifaidika na uporaji huo. Mwanasheria Mkuu wa wakati huo, Jaji Werema, pia alijiuzulu huku wahusika wengine walioshukiwa wakisafishwa na Ikulu.[6] Kuongezeka kwa matukio ya ulaghai, rushwa, na matumizi mabaya ya madaraka yaliyokithiri yanatokana na ukweli kuwa sheria dhidi ya uovu huu zipo isipokuwa changamoto kuu ni utekelezaji na ushurutishwaji wake.[7] Pamoja na hayo, tangu uchaguzi mkuu wa Oktoba 2015 ulipofanyika, Tanzania sasa ina Rais mpya ambaye ana dhamira ya kuwang'amua watumishi wa serikali wanaokula rushwa[8] na vile vile kushughulikia mifumo

isiyo fanisi na inayoliletea hasara taifa ndani ya serikali. Baada ya kuwa madarakani kwa miezi mitatu, Rais Dkt. John Pombe Magufuli ameonesha kwa vitendo kuwa amedhamiria kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kuwa na serikali ambayo inaweza kuaminiwa na wananchi wake, fanisi, na iliyo wazi katika utendaji wake. Rais alianza vyema Urais wake kwa kukata bajeti ya sherehe mojawapo za kitaifa kwa zaidi ya asilimia 90 wakati wa kuzindua bunge na kuamuru fedha zilizookolewa zitumike kununulia vitanda hospitalini. Kitendo hiki kilimfanya apendwe na wananchi wengi, pia kwa sababu alikuwa ameshaanza kupambana na wakwepaji ushuru katika bandari ya Dar es Salaam[9] na kutimiza ahadi yake ya kutoa elimu bure kuanzia ngazi ya msingi hadi sekondari kwa Watanzania wote kuanzia Januari 2016 na kuendelea.

Lakini kuna watu nje ya serikali, hasa mitandaoni, bado wana shaka[10] na baadhi ya hatua zake za hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa au kusimamishwa kazi kwa watumishi waliokuwa hawaleti tija, kama "nguvu za soda". Wanadai kuwa Rais ajikite zaidi katika kuchukua hatua za kuimarisha utawala bora, uadilifu, uwajibikaji, na uwazi katika taasisi na michakato mbalimbali. Wadau wanadai kuwa nchi kutegemea utashi au umahiri wa mtu tu - hapa akilengwa Rais mwenyewe - ni hatari kwa demokrasia na inaweza kutafsiriwa kuwa ni vitu vya kupita tu. Wadau hao, hata hivyo, wamesifu chaguo la Rais la kuwa na baraza la mawaziri dogo ingawa hawakuridhishwa na baadhi ya mawaziri walioteuliwa.

Mmojawapo wa mawaziri walioteuliwa na Rais Magufuli alihusishwa kwenye kashfa zilizopita, ikiwemo ile ya *Tegeta Escrow* mwishoni mwa mwaka 2014. Wachambuzi wengi wameamua kumpa muda Magufuli kwenye cheo chake cha Urais, na kwa ujumla wanamuunga mkono juhudi zake za kuimarisha uwajibikaji wa taasisi, kama ule wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU ambayo mpaka sasa "haina meno".

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inatarajia kuifanya Tanzania kutoka ilipo sasa hadi kuwa nchi ya uchumi wa kati, yenye viwanda na iliyoendelea itakapofika mwaka 2025. Tangu mwaka 2013, Tanzania imetwaa na kutumia modeli mpya ya kuleta matokeo inayoitwa "Matokeo Makubwa Sasa!" (BRN) ili kuhakikisha programu zinatekelezwa kwa wakati, msisitizo ukiwa ni kwa wananchi na ushiriki wao katika utoaji maamuzi. BRN ni modeli iliyoundwa kwa kutumia Mkakati wa Maendeleo wa nchi ya Malaysia, ambayo pia imetwaliwa na kutumika nchini Rwanda na Nigeria. BRN inaelezewa kuwa ni programu pana na kwa Tanzania msisitizo umewekwa kwenye maeneo ya matokeo sita: nishati, kilimo, maji, elimu, usafirishaji na utafutaji rasilimali.

Kwenye elimu, kwa mfano, Tanzania imepiga hatua katika kuandikisha mamilioni zaidi ya watoto kujiunga kwenye Shule za Msingi na Sekondari. Mwaka 2009, kulikuwa na watoto 8,400,000 walioandikishwa kwenye shule za msingi, ikiwa ni ongezeko kutoka idadi ya watoto 7,500,000 walioandikishwa mwaka 2005 na 4,400,000 kwa mwaka 2000. Tangu Elimu ya Msingi itolewe bure nchini (tangu mwaka 2001), watoto 4,000,000 zaidi wameweza kupata elimu.[11] Changamoto iliyopo ni kuboresha mifumo ya elimu ya msingi na sekondari ili kuhakikisha kuwa kujifunza kwa kweli kunawepo kwenye kila darasa.

Mnamo Juni 2015, Bodi ya Wakurugenzi Watendaji wa Benki ya Dunia waliidhinisha mkopo wa jumla ya Dola za Kimarekani 100,000,000 kwa Tanzania kusaidia kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala na kusaidia kuboresha usimamizi wa fedha za umma. Mradi huo wa Sera ya Maendeleo ya Kufungua Serikali na Usimamizi wa Fedha za Umma ni mkopo kwa Tanzania, ulitolewa na *International Development Association* na ni sehemu ya mlolongo wa miradi inayolenga kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma hapa nchini.[12]

Mpango kazi wa pili wa OGP Tanzania unaonesha kuwa serikali imeyatambua vizuri maeneo muhimu ambayo yanahitaji kushughulikiwa. Kutunga sheria ya upatikananji wa taarifa kwa taarifa zinazoshikiliwa na serikali kunaweza kukuza uaminifu kwa umma/wananchi na kusaidia nchi kupambana na rushwa. Mpango kazi wa pili wa OGP Tanzania (2014–16) unaonesha hatua na michakato ambayo itawezesha upatikanaji wa takwimu zinazoshikiliwa na serikali, ikiwa ni pamoja na kuweka wazi taarifa za bajeti, na kushughulikia uwazi katika sekta ya ardhi na tasnia ya uziduaji. Ingawa kuna mafanikio, ni kiasi kidogo tu cha michakato hii ndiyo ipo wazi kwa umma / wananchi kushiriki.

Pale ambapo uhuru wa kujieleza, haki ya raia kupata taarifa, ulinzi kwa raia wema wanaotoa taarifa zinazosaidia kukamatwa kwa wahalifu, na haki ya usiri

wa kila raia zinapohusika, mazingira nchini Tanzania si mara zote yanaruhusu watu wake, wafanyakazi wa vyombo vya habari, na mabloga kufanya majukumu yao ya kuuhabarisha umma bila kuhofu visasi kutoka kwenye vyombo vya dola. Hii inatokana na hivi karibuni kupitishwa kwa miswada miwili, Sheria za Makosa ya Mtandaoni na Takwimu. Upitishwaji huo, uliofanywa kwa hati ya dharura, wa miswada miwili hiyo kuwa sheria ilipofika Septemba Mosi mwaka 2015, kulifikiwa baada ya upinzani mkali dhidi yake.[13] Waharakati wa jamii ya kiraia wamepeleka shauri mahakamani wakijaribu kufuta au kubadili baadhi ya vifungu vyenye utata kwenye sheria hizo.[14]

Wadau wa jamii ya kiraia wanadai kuwa sababu kubwa ya miswada hiyo kupelekwa bungeni chini ya hati ya dharura[15] ilikuwa ni kwa serikali kutaka kuwanyamazisha watu. Sababu nyingine zilitajwa kuwa ni pamoja na serikali kutaka kuzuia uchapishaji wa taarifa ambazo ni nyeti kisiasa ambazo huenda zingeweza kumuathiri mgombea kwenye uchaguzi uliokuwa ukitarajiwa kufanywa. Wadau wa jamii ya kiraia wanadai kuwa chama kinachotawala, yaani Chama Cha Mapinduzi (CCM), huku kikiwa na wabunge wengi, kina uwezo wa kupitisha mswada wowote, hata kama mashauriano na wananchi hayajafanyika au majadiliano ndani ya Bunge hayakufanywa. Wadau wa jamii ya kiraia kwa hiyo wanaonelea kuwa upitishwaji wa miswada hiyo miwili ilikuwa ni jaribio la serikali la kubakiza hali kama ilivyo kisiasa.

Mnamo Julai 2015, bunge pia lilipitisha mswada uliokuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu wa kuwalinda raia wema wanaotoa taarifa zinazosaidia kukamatwa kwa wahalifu na mashahidi. Wasiwasi mkubwa wa baadhi ya wachambuzi[16] ulihusu baadhi ya vifungu ndani ya sheria hiyo, kama vile kuhamasisha utoaji wa taarifa/takwimu, ambao unaweza ukakinzana na sheria inayoonekana kandamizi ya makosa ya mtandaoni ambayo inafanya ushushushu wa takwimu kuwa ni kosa la jinai. Zaidi ya hayo, sheria ya ulinzi kwa raia wema wanaotoa taarifa zinazosaidia kukamatwa kwa wahalifu na mashahidi ya mwaka 2015 haitoi ulinzi moja kwa moja wala kinga kwa raia wema wanaotoa taarifa zinazosaidia kukamatwa kwa wahalifu au mashahidi kwa masuala ya rushwa kwenye sekta ya umma.

Kutokana na sekta za gesi, mafuta na uchimbaji wa madini, Tanzania ilitangazwa rasmi kuwa ni nchi iliyokidhi masharti ya uanachama wa mpango wa kuhamasisha uwazi katika tasnia ya uziduaji (EITI) mnamo tarehe 12 Desemba 2012. Hata hivyo, nchi ilisimamishwa uanachama kwa muda mnamo Septemba 2015 ikiwa ni matokeo ya kushindwa kuchapisha taarifa ya mwaka 2012–13 katika tarehe ya mwisho iliyopangwa, Juni 30, 2015. Kusimamishwa uanachama huko, kulikoma mnamo Desemba 17, 2015 baada ya taarifa za mapato kwa kipindi cha 2012–13 na 2013–14 kuchapishwa mnamo tarehe Novemba 17, 2015.[17] Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya nne ya EITI iliyochapishwa tarehe 30 Juni 2014, mapato ya serikali yanayotokana na tasnia ya uziduaji yaliongezeka kwa asilimia 40 kufikia Dola za Kimarekani 468,000,000[18] kiasi kikubwa kikiwa kimechangiwa na sekta ndogo ya madini.

Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa ya uwazi wa serikali dhidi ya hoja za umma na ushiriki wao, juhudi zaidi zinahitajika kushughulikia fursa ya umma inayozidi kudorora. Kuna haja ya kuondoa hofu miongoni mwa wananchi wanapotafuta au wanapotoa habari kuhusu taarifa za serikali, na pia kuhakikisha usiri wa raia dhidi ya sheria zisizo lazima na kandamizi.[19] Wakati wa mapitio yake mnamo tarehe 3 Oktoba 2011 chini ya Kikao cha 12 cha Kikundi Kazi cha Umoja wa Mataifa (UPR), Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ilikubali mapendekezo 107 yakiwemo yafuatayo: maazimio ya kuendelea kutumia sheria kwa mujibu wa kawaida na misingi ya haki za binadamu (pendekezo nambari 85.4); kuendeleza juhudi za kuhamasisha na kulinda haki za binadamu na uhuru wa raia wake (pendekezo nambari 85.11); na kuhakikisha kuna uhuru wa kujieleza, kujumuika, na kukutana na wengine kwa kuruhusu watetezi wa haki za binadamu, wapinzani kisiasa, na waandishi wa habari kuwa huru kutoa maoni yao kama sheria ya kimataifa juu ya haki za binadamu inavyotamka (pendekezo nambari 85.72).

Pamoja na maazimio haya yaliyo mahsusi, haki ya uhuru wa kujieleza, kujumuika na wengine katika vyama na kukusanyika zinabaki kuwa hatarini - huku watetezi wa haki za binadamu na AzaKi wakifanyiwa visasi kutokana na kufanya kazi zao.[20] Kifungu cha 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinaheshimu uhuru wa kujieleza na maoni ya Watanzania. Kifungu cha 19 cha Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) kinaeleza kuwa "*kila mtu ana haki ya uhuru wa kujieleza; haki hii ijumuishe uhuru wa kutafuta,*

kupokea na kushawishi taarifa na mawazo ya kila aina bila kujali mipaka, iwe kwa maandishi au kuchapishwa, kwa namna ya sanaa, au kwa njia nyingine yoyote ile atakayochagua." Kwa bahati mbaya, haki hii ina masharti kadhaa kama yalivyowekwa na sheria. Haki ya uhuru wa habari nchini Tanzania haiko wazi kwani, baadhi ya sheria zinaikandamiza kama vile Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na ile ya Huduma za Utangazaji ya mwaka 1993 ambazo zinaweza kutumiwa na serikali kufungia au kufuta magazeti na vituo vya televisheni kadri inavyopenda. Mnamo mwezi Januari 2015, gazeti moja la kila wiki, *The East African*, lilifungiwa na mamlaka lisisambazwe/kuuzwa hapa nchini. Katika kutetea ufungiaji huo, mamlaka zilieleza kuwa gazeti hilo halikuwa limesajiliwa rasmi kwa mujibu wa vifungu vya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976.

Hata hivyo, chanzo cha kufungiwa kwa gazeti hilo kunaaminika ni kule kuandika habari za kudhalilisha viongozi serikalini.[21] Mnamo Novemba 2014, Samwel Nangiria, mtetezi wa haki za binadamu na mratibu wa mtandao wa AZISE za wilaya ya Ngorongoro (NGONET), alipokea simu za vitisho na ujumbe mfupi wa maandishi ukimuonya kuhusu kampeni yake ya utetezi kuhusiana na haki ya ardhi kwa Wamasai huko Loliondo, wilayani Ngorongoro. Samwel bado anaendelea na juhudi dhidi ya uamuzi uliochukuliwa na Wizara ya Utalii kutenga kitalu cha kilometa za mraba 1,500 kwa kampuni moja ya uwindaji yenye maskani yake huko Dubai,inayoitwa *Otterlo Business Corporation*. Uamuzi wa kuwaondoa Wamasai ulifikiwa kwa kupindua uamuzi mwingine wa awali kwa juhudi zilizoongozwa na kutetewa na AzaKi wa kulinda ardhi ya wachungaji wa Kimasai waliyoirithi kutoka kwa mababu zao. Kigeugeu hicho kikapelekea familia za Kimasai 80,000 kukosa mahali pa kuishi na kuwanyima kupata ardhi, malisho na maji.

Ni katika muktadha huu wa kijamii na kisiasa ambapo mpango kazi wa OGP uliandaliwa na kutekelezwa.

VIPAUMBELE VYA WADAU

Bado serikali ya Tanzania inatakiwa kuboresha zaidi utekelezaji iliyoufanya kwa mpango kazi wa pili, na ijidhatiti kwenye mchakato wa OGP.

Wakati wa kuandaa mpango kazi ujao, wadau wa jamii ya kiraia wanaamini kuwa masuala yafuatayo lazima yafikiriwe:-

- **Chombo cha uangalizi na taarifa za maendeleo:** Serikali iliunda tovuti kuu ya OGP (ambayo sasa inapatikana http://www.opengov.go.tz). Pamoja na hayo, hakuna kamati ya uangalizi iliyopewa jukumu la kushughulikia tovuti kuu hiyo na taarifa zilizomo hazijahuishwa kwa kila robo mwaka kama ilivyoahidiwa. Taarifa kuhusu utekelezaji wa maazimio ya OGP hayapatikani kwenye tovuti kuu hiyo. Ukosefu wa taarifa za mara kwa mara - kila mwezi, robo mwaka, na za mwaka - zinaleta dhana kuwa jukumu la kuratibu ukusanyaji takwimu au taarifa na kuchapisha mtandaoni halikukabidhiwa kwa taasisi yoyote kulitekeleza.
- **Serikali za mitaa:** Mpango kazi unahamasisha ufunguaji serikali kwa kuzitaka taasisi za serikali kuchapisha takwimu zao kwenye tovuti kuu ya takwimu huria na kubandika matangazo katika ngazi ya vituo vya huduma. Serikali haina budi kuweka vipaumbele vya namna serikali za mitaa zitakavyoshiriki kwenye mkakati wa OGP na kuhamasisha zaidi utekelezaji wa maazimio yote kama vile uchapishaji wa takwimu za bajeti, uwazi katika masuala ya ardhi na tasnia ya uziduaji na kadhalika.
- **Kutangaza mali na madeni ya watumishi wa umma:** Wadau wa jamii ya kiraia wanaamini kuwa serikali lazima ichukue hatua ambazo zitawafanya viongozi wawajibike kwa wananchi, kama vile kuandaa mswada utakaokuwa shirikishi na wazi kwa watumishi kutangaza mali na uhalali wa michakato ya kidemokrasia wakati wa kutunga sheria nchini Tanzania.[22] Azimio kama hii lilikuwa sehemu ya mpango kazi wa kwanza, ingawa hakukuwa na utekelezaji, na serikali haikuliweka tena azimio hilo kwenye mpango kazi wa pili pamoja na mapendekezo ya mtafiti wa IRM. Hili ni muhimu, hususan katika zama hizi ambapo viongozi wa juu wa serikali wanatuhumiwa kwa rushwa.[23] Kwa mujibu wa Kipimajoto cha Rushwa Duniani - *Global Corruption Barometer* cha mwaka 2013, asilimia 75 ya Watanzania walisema maafisa wa serikali na watumishi wengine wa umma walikuwa wala rushwa au wala rushwa wakubwa.[24]
- **Uchapishaji taarifa kwa Kiswahili:** Serikali na wadau wengine wa OGP nchini Tanzania mara nyingi wameshindwa kutambua kuwa na rasimu za

mipango kwa Kiswahili, na kufanya mchakato wa utoaji maoni kuwa wazi kwa umma, kunaweza kutia moyo wa ushiriki na kusaidia kujulikana kwa OGP na wadau wengi mbalimbali.

Wakati wa mkutano na wadau wa jamii ya kiraia, ilipendekezwa kuwa maazimio yote yaliyopo sasa yanayohusiana na upatikanaji wa taarifa zinazoshikiliwa na serikali, michakato ya wazi ya bajeti na kutangaza mikataba kuhusu ardhi na tasnia ya uziduaji ibakizwe kwenye mpango kazi ujao wa OGP nchini Tanzania.

WIGO WA MPANGO KAZI UKIHUSISHWA NA MUKTADHA

Wadau wa jamii ya kiraia walisisitiza haja ya serikali kujumuisha lugha bora za kuhamasisha mwingiliano na wananchi na uhusika wa jamii ya kiraia katika mpango kazi ujao. Maazimio hayana budi kuwa na utashi wa kutosha kuiwezesha serikali ya Tanzania kuwa wazi zaidi, ya kuaminika na sikivu kwa wananchi wake.

Wadau pia wameomba kuwa utangazaji wa mali za watumishi wa umma libakie kama mojawapo ya azimio la lazima pamoja na azimio jipya la kubadili sheria ambazo zinaenda kinyume na haki za msingi za binadamu, kama vile sheria zilizopitishwa karibuni za Makosa ya Mtandaoni na Takwimu – ambazo zinaenda kinyume na misingi ya uwazi yaOGP, uwajibikaji, ushiriki wa wananchi katika kuendesha serikali yao na matumizi ya teknolojia kwa kuimarisha michakato ya uwazi na uwajibikaji.

Baadhi ya wadau walielezea masikitiko yao kwa kile kilichoonekana katika maazimio ya uwajibikaji ambapo mara nyingi serikali imekuwa ikishindwa kukamilisha utekelezaji wa maazimio hayo ya OGP, wakinyooshea kidole kushindwa kutekelezwa kikamilifu kwa azimio la kwanza la mpango kazi uliopo wa OGP juu ya upatikanaji taarifa za serikali na azimio lingine linalohusu kutangaza mali za watumishi wa umma lililokuwemo kwenye mpango kazi uliopita, kama ushahidi.

Wadau wa jamii ya kiraia pia walipendekeza kuwa maazimio yaunganishwe kutokana na dhamira ya makundi yanayoendana na tunu mahsusi za OGP, kama vile upatikanaji wa taarifa, uwajibikaji kwa umma, na ushiriki wa wananchi. Hata hivyo, mtafiti wa IRM haamini kuwa uunganishaji maazimio unaweza kuboresha utekelezaji wa azimio mojamoja kama yalivyo sasa. Mtafiti wa IRM anaamini kuwa endapo maazimio yaliyopo sasa hayatatekelezwa kwa kipindi hiki cha utekelezaji, baadhi yao kama ilivyopendekezwa, yanaweza kuingizwa kwenye mpango kazi ujao.

---

[1] National Anti-corruption strategy in Tanzania, Anti-Corruption Resource Centre, http://bit.ly/1SIzgQ9
[2] A country's rank indicates its position relative to other countries in the index and the score indicates the perceived level of public sector corruption on a scale of 0 to 100 (from the highly corrupt to very clean). http://bit.ly/1vJVF4W
[3] http://www.transparency.org/whatwedo/answer/overview_of_corruption_and_anti_corruption_in_tanzania
[4] Business Corruption in Tanzania. May 2015. http://bit.ly/1mkq6oW
[5] Kizito Makoye. Donors freeze aid to Tanzania. October 16, 2014 http://bit.ly/20aaIAhpage accessed on 20 January 2016
[6] Athuman Mtulya. 'Tegeta escrow will go down in history as a major scandal'. January 1, 2015. http://bit.ly/1ZCmK4Zpage accessed on 20 January 2016
[7] Business Anti-Corruption Portal, 2015
[8] Katare Mbashiru. TRA chief Bade axed in Magufuli tax crackdown. November 28,2015. http://bit.ly/1P7QNyO; and Devotha Mwachang'a. Magufuli dissolves TPA board over scandals suspends 12 bigwigs. December 8, 2015. http://bit.ly/1S1sjenpages accessed on 20 January 2016
[9] Katare Mbashiru. 9bn/- collected at TRA as container owners pay up. 8 December, 2015. http://bit.ly/1UM5RUn and Erick Kabendera. Tanzania: Magufuli Tax Evasion Crackdown Yields Fruit. December 13, 2015 http://bit.ly/1X4oqo8pages accessed on 20 January 2016
[10] Author's/IRM researcher's own interaction on his twitter handle @Hembeti
[11] URT. Basic Education Statistics in Tanzania (BEST) 2005-2009, Ministry of Education & Vocational Training, July 2009
[12] World Bank Mobilizes US$100 million to Promote Transparency and Open Governance Reforms in Tanzania. June 23, 2015. http://bit.ly/1meGsXp accessed on 20 January 2016
[13] Four bills later: is blogging with statistics in Tanzania now only for adrenalin junkies? 25 March, 2015, Mtega, http://bit.ly/1yGGS9p
[14] Parts of Cybercrime Act opposed in court, 12 September, 2015, The Citizen, http://bit.ly/23JHfSq
[15] Under the certificate of urgency, a Bill can be sent to parliament with little or no public consultation, minimal or no debate inside parliament to being voted in approval of its unknown/uninformed contents.
[16] Parts of Cybercrime Act opposed in court, 12 September, 2015, The Citizen, http://bit.ly/23JHfSq
[17] Tanzania: More revenues from extractives despite falling prices, 17th December, 2015, http://bit.ly/1PVdrhB accessed 15 January 2016
[18] Extractives Industries Transparency Initiative, Tanzania https://eiti.org/Tanzania accessed on 20th October 2015.
[19] Fears Over Tanzania's Cybercrime Law Become Reality During Presidential Election, 29 October 2015, Slate, http://slate.me/1k1vpQo
[20] CIVICUS, THRDC and TANGO. Extract from "Joint Submission to the UN Universal Periodic Review 25th Session of the UPR Working Group United Republic of Tanzania". September 21, 2015
[21] Tanzania bans "the East African" over coverage of government registration The East African http://bit.ly/1o7LBCi, accessed 26 August 2015
[22] Revealed: Tanzanians' Sh205bn in Swiss banks, 10 February, 2015, The Citizen, http://bit.ly/20aaWqX
[23] Revealed: Tanzanians' Sh205bn in Swiss banks, 10 February, 2015, The Citizen, http://bit.ly/20aaWqX
[24] Transparency International: Tanzania, http://bit.ly/20ab2yY

VII | MAPENDEKEZO YA JUMLA

MAPENDEKEZO MTAMBUKO

Mtafiti wa IRM anapendekeza kuendelea kuwa na mpango kazi wa miaka miwili na kuweka msisitizo kwa maazimio mahsusi huku matokeo tarajali kwa kila azimio yakiwa yanaeleweka na yanapimika. Msisitizo katika mpango kazi ujao ni kufanya takwimu au taarifa zinazoshikiliwa na serikali zipatikane kwa wananchi. Pia, uwazi katika sekta kama vile ya uziduaji na kutangaza mali za watumishi wa umma zipewe kipaumbele cha juu kwenye mpango kazi ujao wa OGP.

MCHAKATO WA OGP

1. **Michakato ya mashauriano:** Ili kuimarisha ushiriki wa wadau kwenye mchakato wa OGP, serikali ianzishe mfumo wa mazungumzo kusaidia uangalizi wa hatua za utekelezaji na uwajibikaji bora zaidi kwa taasisi zinazotekeleza maazimio. Takwimu zote zinazotolewa zitafsiriwe kwa Kiswahili ili kuwezesha upatikanaji wake nchi nzima. Mchakato wa mashauriano ulenge katika kufikia uwazi wa mchakato na uwepo wa notisi na kujenga weledi wa kutosha kwa wananchi.
2. **Mawasiliano ya hatua zilizofikiwa mtandaoni:** Matumizi ya tovuti kuu iliyopo, kutoa taarifa za maendeleo ya utekelezaji na kuhakikisha uhuishaji wa mara kwa mara juu ya maendeleo kwa ujumla ya utekelezaji wa OGP hapa www.ega.go.tz/ogp, kinadharia, ingependeza ikiwa chini ya kitengo cha Mitandao ya Serikali.
3. **Mtu wa kuwasiliana wa serikali:** Iwekwe taasisi kiongozi na jina la mtu wa kuwasiliana naye kwenye mpango kazi kwa kila azimio ili wananchi waweze kuwasiliana nao, pia kutoa fursa kwa wananchi kuuliza maswali ya kutaka kujua zaidi au taarifa za ziada watakazotaka.
4. **Uchapishaji wa taarifa:** Kuhakikisha kuwa taarifa zote za utekelezaji kuhusiana na OGP zinawekwa kwenye tovuti kuu ya OGP, huku ikielekeza kwenye tovuti za wizara, idara na wakala wa serikali, na pia kupatikana kwa nakala halisi ya taarifa hizi kwa ngazi zote za serikali hadi vituoni, kwa wakati.

MAAZIMIO

1. **Upatinakaji taarifa:** Bila kukawia, serikali ipeleke bungeni rasimu ya mswada wa sheria ya upatikanaji wa taarifa za serikali kwa kuhakikisha yafuatayo: (a) kuwa mashauriano sahihi yanafanyika, (b) kuwa mswada huo utapelekwa bungeni kipekee ili upitishwe, na (c) unaendana na vigezo vya kimataifa, huku ikiweka bayana utoaji taarifa bila ukomo kama msingi muhimu wa haki ya kupata taarifa. Pia, mswada hauna budi uweke chombo cha usimamizi kuhakikisha utekelezaji wake.
2. **Uchapishaji takwimu:** Ili kuenzi dhamira ya serikali ya kutoa takwimu huria na uwazi katika bajeti, taarifa za kila robo mwaka na misamaha ya kodi iliyotolewa kwenye sekta za elimu, afya na maji ni lazima zichapishwe kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha kwa wakati. Kwa kufanya hivi, takwimu zilizochapishwa zitakuwa na maana na serikali itafaidika na mrejesho na michango zaidi kutoka kwa watumiaji. Hili pia litakuza ushiriki wa wananchi na kuwezesha uanzishwaji wa mifumo ya uawajibikaji wa serikali kwa wananchi.
3. **Serikali za mitaa:** Kujumuisha ushiriki wa mamlaka za serikali za mitaa katika utekelezaji wa maazimio ya OGP, hasa yale yanayohusu kuweka bajeti zilizopitishwa, fedha zilizotumwa/kupokelewa na taarifa za utekelezaji kwenye mbao za matangazo mpaka ngazi ya vituo vya huduma na sehemu nyingine za umma.
4. **Kutangaza mali za watumishi wa umma:** Serikali iandae marekebisho ya sheria na kanuni huku ikihakikisha kunakuwa na mashauriano mapana ili kuimarisha utangazaji wa mali za watumishi wa umma. Ni muhimu kuandaa mwongozo wa hatua kwa hatua na uwekwe wazi kwa wananchi kuhusiana na viongozi gani wa juu/waandamizi wanaolazimika kutangaza mali zao. Taarifa za mali na madeni hazina budi kupatikana kwa umma, ikiwa ni pamoja na kutumia njia nje ya mtandao kama vile gazeti rasmi la serikali. Azimio hili liwe ni sehemu ya mpango kazi ujao wa OGP nchini Tanzania.
5. Masuala kama kilimo, changamoto zinazoletwa na mabadiliko ya tabia nchi na masuala ya haki ya wanawake kumiliki ardhi yaingizwe kwenye azimio linalohusu uwazi katika masuala ya ardhi, endapo serikali itashindwa kukamilisha utekelezaji wake katika muda wa mpango kazi uliopo.

MAPENDEKEZO MAKUU MATANO
1. **Mchakato wa mashauriano wakati wa kuandaa mpango kazi unahitaji kuwa wazi zaidi.** Serikali inaweza kuboresha juhudi za kujenga weledi kwa kuufahamisha umma kuhusu muda, mfumo na mchakato kwa ujumla. Takwimu zinazotolewa kwa matumizi ya umma zitafsiriwe kwa Kiswahili kuruhusu upatikanji wa taarifa kwa nchi nzima.
2. **Kuanzisha mfumo rasmi wa majadiliano utakaowezesha usimamizi wa utekelezaji na kuhakikisha uwajibikaji kwa wakala zinazohusika na utekelezaji wa maazimio.**
3. **Bila ya kukawia, serikali ipeleke mswada bungeni wa sheria ya upatikanaji wa taarifa** ikizingatia yafuatayo: (a) kwamba majadiliano ya dhati yanafanyika, (b) kwamba inapelekwa bungeni ili bunge liridhie kuwa sheria, na (c) sheria hiyo iendane na sheria zingine za mfano kimataifa.
4. **Serikali iandae marekebisho ya sheria na kanuni ili kuimarisha dhamira ya kutangaza mali na madeni ya watumishi wa umma.**
5. **Serikali ianzishe jukwaa la wazi ambamo wananchi/watumiaji wa takwimu za serikali wanaweza kuzipata kirahisi au kuwasiliana nao ikiwa ni pamoja na kuunda mifumo ya kupata mrejesho wa watumiaji takwimu ili kuwepo na ushiriki wa wananchi hata katika ngazi ya serikali za mitaa.**

VIII | METHODOLOJIA NA VYANZO

Kama heshima kwa taarifa ya serikali ya kujitathmini, taarifa nyingine huru ya IRM huandikwa na watafiti wanaoaminika kuwa wanafahamu vyema masuala ya utawala/uongozi, hasa wale wanaoishi katika nchi husika inayoshiriki OGP.

Wataalamu hawa wanatumia dodoso na miongozo ya OGP inayotumika hata kwa nchi zingine,[1] ikijikita kwenye mchanganyiko wa mahojiano na wadau wa OGP nchini na pia uchambuzi unaotokana na utafiti mtandaoni. Taarifa hii hupelekwa kwenye jopo dogo la wataalamu wa kimataifa (lililoteuliwa na Kamati Elekezi ya OGP kimataifa) ili kupitia kwanza na kuhakikisha vigezo vyote vya utafiti vimefuatwa kwa umakini wa hali ya juu na pia kila hatua ya kuthibitisha imefuatwa.

Uchambuzi wa maendeleo ya utekelezaji wa mpango kazi wa OGP ni mchanganyiko wa mahojiano, utafiti mtandaoni, na mrejesho kutoka kwenye mkutano wa wadau walio nje ya serikali. Taarifa ya IRM hutumia matokeo ya taarifa ya serikali ya kujitathmini na tathmini nyingine yoyote iliyofanywa na jamii ya kiraia, sekta binafsi au asasi/mashirika ya kimataifa.

Kila mtafiti anaitisha mkutano na wadau ili kuhakikisha matukio yanayotaarifiwa yana usahihi. Sababu ya changamoto za kifedha na mgongano wa kalenda, IRM haiwezi kuhoji/kuwafikia wote ambao wangependa kushiriki au walioathirika. Mwishowe, IRM inajitahidi kuwa na uwazi wa methodolojia yake, na hivyo pale inapowezekana, huweka wazi mchakato wa namna wadau walivyohusika kwenye utafiti (imeelezwa kwa kina baadaye katika sehemu hii.) Kwenye muktadha kadhaa kitaifa ambapo wahojiwa huomba kutotajwa - wawe ni kutoka serikalini au nje - IRM ina uwezo wa kulinda usiri huo wa wahojiwa. Pia, kwa sababu ya mipaka ya methodolojia iliyotumika, IRM inakaribisha kwa dhati maoni kwa rasimu ambayo iko wazi kwa wananchi kutoa taarifa mbalimbali zinazohusiana na nchi.

MAHOJIANO NA VIKUNDI VYA MAJADILIANO

Mtafiti wa IRM nchini Tanzania alifanya mkutano mmoja wa wadau kwa kualika mchanganyiko wa wawakilishi wa jamii ya kiraia na wengine nje ya sekta za dola ambao walikuwa wakifahamu OGP nchini Tanzania na wale ambao hawakujua kabisa OGP ni nini. Pia, mtafiti wa IRM alifanya mahojiano ya ana kwa ana, kwa njia ya simu na kutafuta ushahidi kwa njia ya mapitio mtandaoni na maombi kwa baruapepe.

Kwa vile serikali haikuandaa taarifa yake ya kujitathmini ya kila mwaka (ni lazima waandae), kulikuwa na umuhimu wa mtafiti wa IRM kuzihoji taasisi viongozi na saidizi kwa kila azimio kati ya yale matano ili kunakili au kupata taarifa zaidi ya zile zilizopo mtandaoni. Ni baadhi tu ya wawakilishi wa serikali waliotambulishwa kwa mtafiti wa IRM ndio walipatikana kwa mahojiano, hivyo kulazimisha mtafiti kutafuta vyanzo vingine wakiwemo wahojiwa nje ya serikali au kutafuta taarifa husika mtandaoni.

Mtafiti wa IRM alifanya mahojiano na maofisa wa serikali kwa njia za ana kwa ana na mahojiano kwenye simu. Ieleweke kwamba, katika mchakato wa utafiti/tathmini hii, mtafiti wa IRM alikuwa na haki ya kuficha sura/utambulisho wa maafisa wa serikali na wadau nje ya serikali waliohojiwa ili maoni yaweze kutolewa kwa uwazi zaidi na kuwalinda wahojiwa hao dhidi ya hatari ya visasi. Katika taarifa hii, baada ya kuombwa na baadhi ya wahojiwa, sura/utambulisho wa vyanzo vya mahojiano zimefichwa kwa sababu zilizoelezwa hapo awali.

Kupitia mahojiano ya awali na sekretarieti ya OGP, mtafiti wa IRM aliweza kuzitambua AzaKi ambazo zinashiriki kama sehemu ya Kamati Elekezi kitaifa ya OGP, zimeshiriki katika kuandaa mpango kazi au zilihusika katika utekelezaji wa maazimio. Kisha, mtafiti wa IRM akatuma mialiko kwa baruapepe na kufuatilia kwa simu ili kupata tarehe na muda muafaka wa kufanya mkutano wa wadau kama kikundi cha mahojiano.

Tarehe ya kukamilisha taarifa hii ya IRM ilikuwa ni Oktoba Mosi 2015, na kwa kuwa huo ulikuwa ni mwezi na mwaka wa uchaguzi nchini Tanzania, kulisababisha changamoto kubwa za kukubaliana tarehe ya kufanya mkutano huo wa wadau - kwani mara nyingi ziligongana na majukumu ya wadau kwenye mchakato wa uchaguzi. Hivyo, mtafiti wa IRM akaambulia kufanya mkutano mmoja tu uliofanyika Dar es Salaam, mnamo tarehe 25 Septemba 2015.

Washiriki walikuwa ni wadau nje ya dola, ambapo mwanzoni mtafiti wa IRM alikuwa na orodha ya washiriki tarajali ishirini (20). Kumbi tatu zilitafutwa kabla ya kukubaliana na mojawapo. Washiriki tarajali walipigiwa simu na kutumiwa baruapepe. Kwa sababu ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 nchini, ni washiriki kumi tu ndio walioweza kushiriki mkutano huo. Washiriki walitambuliwa kwa kutazama uzoefu wao kwenye masuala ya utawala/uongozi au kwa kuwa waliwahi kushiriki kwenye mikutano kama hii huko nyuma. Pia, baadhi yao walikuwa ni wanachama wa AzaKi ambazo zinafahamu au kuhusika na OGP nchini Tanzania. Kigezo kingine kilichotumika kuwapata washiriki wa mkutano huo ni mchanganyiko wa marika ya watu (mfano, vijana, wanawake na watu wenye ulemavu) na ujasiriamali. Njia ya majadilaino kwa vikundi ilimaanisha kwamba idadi isizidi hiyo ili kuwa na ushiriki wa tija kwa wahudhuriaji wote. Mtafiti wa IRM alihakikisha kuwa angalau 4 kati ya washiriki hao walikuwa ni wanawake.

Ni washiriki 4 tu ndio waliokuwa wakiifahamu dhana ya OGP na michakato yake hapa Tanzania.

Washiriki walipitia mchakato wa uundaji wa mpango kazi, kupima kiwango cha weledi kwa wananchi, na endapo/au la kama kulikuwa na mashauriano kabla na wakati wa utekelezaji wa maazimio. Pia, walipitia majukumu na uhusika/ushiriki wa jamii ya kiraia katika mchakato wote. Kwa kuongozwa na mtafiti wa IRM, washiriki walipitia mpango kazi wa pili wa OGP, uliokuwa na maazimio matano. Washiriki waliombwa kupima kiwango cha utekelezaji, utashi, umuhimu kwa OGP na manufaa ya kila azimio.

Washiriki walitumia muda mwingi wakijadili hasa maazimio manne, ambayo ni 3.1, 3.3, 3.4, na 3.5. Walimpatia mtafiti wa IRM vyanzo mbadala vya kupima maazimio kwa maeneo yaliyosisitizwa na pia kutoa mapendekezo kwa kila azimio. Majadiliano hayo pia yaliipatia IRM taarifa nyingi muhimu, hasa pale muktadha wa OGP kitaifa unapohusika. Hatimaye, washiriki walitakiwa kutoa mapendekezo mahsusi kwa kila azimio kati ya yale maazimio matano na mapendekezo ya ujumla kwa mpango kazi ujao wa OGP nchini Tanzania.

Wafuatao ni watendaji nje ya dola ambao walihudhuria mkutano wa mjadala kwa vikundi:

- Grace Mnzava (asasi ya Forum for Grassroots Development Tanzania)
- Tatu Masangula (asasi ya Bagamoyo Education Development Foundation)
- Bautista Mgomba (Shirikisho la Vyama vya Walemavu Tanzania - SHIVYAWATA[2])
- Bakar Khamis (Finnish Centre for International Cooperation, KEPA)
- Anna Pius (Mama Lishe)
- Shomari Pembe (asasi ya Coastal Youth Vision Association)
- Agnes Junga (National CSO HIV/AIDS, National Steering Committee NSC)
- Dr. Andrew Mushi PhD (mwanazuoni Chuo Kikuu cha Mzumbe)
- Abdallah Makungu (Mhasibu na mtalamu wa TEHAMA)
- Hassan Karanda (asasi ya Community-Oriented Development Action - CODATz)

MAKTABA YA MAKABRASHA DOCUMENT LIBRARY

IRM hutumia maktaba za wazi zinazoweza kufikiwa na mtu yeyote zilizopo mtandaoni kama hazina ya taarifa zilizokusanywa kwa kipindi chote cha mchakato wa utafiti. Taarifa yote halisia, na vilevile taarifa kadhaa zilizofanyiwa rejea kwenye taarifa hii, yanapatikana kwa ajili ya kusoma na kutoa maoni kwenye maktaba ya mtandaoni ya IRM kwa Tanzania, hapa http://bit.ly/1zLrV50.

KUHUSU MFUMO HURU WA TAARIFA ZA OGP

IRM ni njia muhimu ambayo kwayo serikali, AzaKi na sekta binafsi zinaweza kufuatilia uandaaji na utekelezaji wa mipango kazi ya OGP kwa kila miaka miwili. Upangiliaji wa utafiti na kuhakiki ubora wa taarifa hizo hufanyika na jopo la wataalamu kimataifa – *International Experts' Panel*, linaloundwa na watu waliobobea kwenye masuala ya uwazi, ushirikishaji, uwajibikaji, na njia za kiutafiti za sayansi ya jamiii.

Wajumbe wanaotumikia jopo la wataalamu kimataifa kwa sasa ni:

- Anuradha Joshi
- Debbie Budlender
- Ernesto Velasco-Sánchez
- Gerardo Munck
- Hazel Feigenblatt
- Hille Hinsberg
- Jonathan Fox
- Liliane Corrêa de Oliveira Klaus
- Rosemary McGee
- Yamini Aiyar

Kundi dogo la wafanyakazi waliopo jijini Washington, DC, wanatunza taarifa hizi na kuratibu michakato ya tathmini kupitia mchakato wa IRM kwa ushirikiano wa karibu kabisa na mtafiti. Maswali na maoni juu ya taarifa hii ya tathmini ya IRM yaelekezwe kwa wafanyakazi kupitia baruapepe hii irm@opengovpartnership.org

[1] Mwongozo kamili unapatikana kwenye kitini cha utaratibu cha IRM, hapa: http://www.opengovpartnership.org/about/about-irm
[2] Muungano wa vikundi/AzaKi za walemavu nchini Tanzania

IX I KIAMBATANISHO JUU YA MASHARTI YA USTAHIKI

Mnamo Septemba 2012, OGP iliamua kuanza kwa kuhamasisha serikali za nchi zinazoshiriki kutwaa na kutumia maazimio yenye utashi ukilinganisha na vigezo vya kukubaliwa kushiriki OGP.

Kitengo cha msaada kwa OGP kinakusanya na kuweka pamoja vigezo vya ukubalifu kila mwaka. Alama hizi zinaoneshwa hapa chini. Pale inapobidi, taarifa za IRM huongelea muktadha unaoonesha kupiga hatua au kurudi nyuma kwa vigezo mahsusi katika sehemu ya muktadha kitaifa.

Kigezo	2011	Ilivyo sasa	Badiliko	Maelezo
Uwazi katika Bajeti[2]	4	4	Hakuna	4 = Muhtasari wa Mapendekezo ya Bajeti na Taarifa ya Ukaguzi zinachapishwa 2 = Moja kati ya hivyo viwili inachapishwa 0 = Hakuna inayochapishwa
Upatikanaji wa taarifa[3]	3	3	Hakuna	4 = Sheria ya upatikanaji wa taarifa (ATI) ipo 3 = Katiba ina kipengele cha ATI 1 = Rasimu ya sheria ya ATI ipo 0 = Hakuna sheria ya ATI
Kutangaza mali[4]	2	2	Hakuna	4 = Sheria ya kutangaza mali ipo, takwimu zinatolewa kwa umma 2 = Sheria ya kutangaza mali ipo, takwimu hazitolewi kwa umma 0 = Sheria haipo
Ushiriki wa umma/ wananchi (Alama ghafi)	3 (5.29)[5]	3 (5.59)[6]	Hakuna	*EIU Faharasa ya Ushirikishwaji wa Wananchi alama ghafi:* 1 > 0 2 > 2.5 3 > 5 4 > 7.5
Jumla / Inayowezekana (Asilimia)	12/16 (75%)	12/16 (75%)	Hakuna	Asilimia 75 ya pointi ambazo zingeweza kupatikana ili kustahiki

[1] For more information, see http://www.opengovpartnership.org/how-it-works/eligibility-criteria
[2] For more information, see Table 1 in http://internationalbudget.org/what-we-do/open-budget-survey/. For up-to-date assessments, see http://www.obstracker.org/
[3] The two databases used are Constitutional Provisions at http://www.right2info.org/constitutional-protections and Laws and draft laws http://www.right2info.org/access-to-information-laws
[4] Simeon Djankov, Rafael La Porta, Florencio Lopez-de-Silanes, and Andrei Shleifer, "Disclosure by Politicians," (Tuck School of Business Working Paper 2009-60, 2009): http://bit.ly/19nDEfK; Organization for Economic Cooperation and Development (OECD), "Types of Information Decision Makers Are Required to Formally Disclose, and Level Of Transparency," in Government at a Glance 2009, (OECD, 2009). http://bit.ly/13vGtqS; Ricard Messick, "Income and Asset Disclosure by World Bank Client Countries" (Washington, DC: World Bank, 2009). http://bit.ly/1clokyf; For more recent information, see http://publicofficialsfinancialdisclosure.worldbank.org. In 2014, the OGP Steering Committee approved a change in the asset disclosure measurement. The existence of a law and de facto public access to the disclosed information replaced the old measures of disclosure by politicians and disclosure of high-level officials. For additional information, see the guidance note on 2014 OGP Eligibility Requirements at http://bit.ly/1EjLJ4Y
[5] Economist Intelligence Unit, "Democracy Index 2010: Democracy in Retreat" (London: Economist, 2010). Available at: http://bit.ly/eLC1rE
[6] Economist Intelligence Unit, "Democracy Index 2014: Democracy and its Discontents" (London: Economist, 2014). Available at: http://bit.ly/18kEzCt

Independent Reporting Mechanism
Open Government Partnership
c/o OpenGovHub
1110 Vermont Ave NW Suite 500
Washington, DC 20005

Open Government Partnership
INDEPENDENT REPORTING MECHANISM